

Jiunge Nasi
Katika

Siku za
MAOMBI

10

**Kutafuta
Uamsho**

Yeremia 29:13

Janury 6 - 16, 2021

WWW.TENDAYSOFPRAAYER.ORG



Ujumbe kutoka NTUC na STUM

Kwa waumini wa kanisa la Waadventista wa Sabato katika Northern Tanzania Union Conference na Southern Tanzania Union Mission, na nje ya Union hizi; tunawataki Amani, Baraka na furaha, moyo wa kumpenda Mungu na kumtumikia mnapopitia masomo haya ya ‘Siku kumi za maombi’ kwa mara nyingine tena.

Hatuna budi kumshukuru Mungu kwa jinsi alivyotulinda tangu Januari mwaka jana (2020) tulipokuwa na program hizi. Mungu wetu apewe sifa. Tunawashauri viongozi wa makanisa wahamasishe waumini kushiriki kikamilifu katika program ya maombi ya mwaka huu bila kukosa, kila siku na kwa wakati ili wote wahesabiwe katika wale watakaopokea mibaraka itakayoandamana na maombi haya. Kanisa mahalia lipange muda muafaka kadiri inavyowezekana, utakaowawezesha waumini wote pamoja na wageni kuhudhuria.

Ikiwezekana kila Conference au field ibuni namna ya kufanya juma hili liwe ni juma la pekee na la kuvutia. Ili kufanya program hii iwe na mguso mkubwa wa kiroho, tunashauri zoezi hili lifanyike kwa kubadilishana wahudumu kanisa moja na jingine au mtaa kwa mtaa. Ikiwa kuna visa vyovyyote vya namna Mungu alivyodhihirisha uwezo wake kwenye jumuiya ya waumiini (kanisa) au kwa mtu mmoja mmoja katika siku hizi kumi za maombi, basi visa hivyo vitumwe Union kupitia kwa Makatibu wa Chama cha Wachungaji wa Conference mahalia ili viunganishwe na visa vya sehemu zingine duniani. Bwana awabariki mnapopitia masomo haya na kuyaweka katika uzoefu. Taarifa hizi zitufikie ndani ya mwezi wa January 2021.

Masomo haya yameandaliwa na Kitengo cha Uchungaji (Ministerial) - ‘Siku Kumi za Mombi’- cha Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato (GC) na kuhaririwa na Makatibu wa Chama cha Wachungaji wa Union mbili za Tanzania ambao ni, Pastor Daniel Ndiegwi wa NTUC na Pastor Hebert Nziku wa STUM. Yametafsiriwa na Moseti Chacha wa kanisa la Waadventista wa Sabato la Lemara.

Ni sisi Wajoli wenu

Pastor Daniel Ndiegwi

Simu: +255 767 543 904 / 784 543 904

Baruapepe: dndiegwi@yahoo.com

Pastor Hebert Nziku

Simu: +255 764 150 378 / 677 150 378

Baruapepe: nzikulihove@gmail.com

YALIYOMO:

Kutafuta Uamsho - Mwongozo wa Kiongozi	3
Utangulizi	9
Usiku wa Maombi	14
Changamoto za Kuwafikia watu walio nje	16
Ahadi za Kudai kwenye Maombi	19
Sherehe ya Siku ya Sabato ya Mwisho	27
Mahitaji ya Kuombea ya Kanisa la Kiulimwengu	29
Siku ya 1 - Zawadi ya Yesu ya Pekee zaidi	33
Siku ya 2 - Kushikilia Zawadi	36
Siku ya 3 - Ufunguo ni Kujisalimisha	39
Siku ya 4 - Kuweka Uamsho Katika Utendaji	43
Siku ya 5 - Kuwa Wa Kiroho au wa Kimwili	47
Siku ya 6 - Ufumbuzi wa Mungu kwa Mahangaiko Yetu	51
Siku ya 7 - Kuomba Ahadi za Mungu	55
Siku ya 8 - Utii Kupitia kwa Yesu	59
Siku ya 9 - Je, Ninafanya kazi kwa ajili ya Mungu?	63
Siku ya 10 - Kutafuta Uamsho Pamoja	67

KUTAFUTA UAMSHO

MWONGOZO WA KIONGOZI

Karibu katika Siku Kumi za Maombi mwaka 2021! Tunaamini maombi ndipo mahali uamsho unapozaliwa. Mungu ametenda miujiza mgingi katika miaka iliyopita kadiri tulivyokuwa tukimtafuta katika maombi na kufunga. Roho Mtakatifu amewezezesha uamsho, mabadiliko, hisia za uinjilisti zilizojengwa upya, makanisa yaliyoamshwa, na mahusiano yaliyoponywa.

Je, sauti ya Mungu imekuwa ikikuita kufanya uamsho?

Biblia imejaa ahadi kwa ajili yako:

“Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao” (*2 Nyakati 7:14*).

“Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote” (*Yeremia 29:13*).

“Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliita jina la Bwana ataponywa” (*Yoeli 2:32*).

“Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi” (*Yakobo 4:8*).

“Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlanga, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na ye ye pamoja nami” (*Ufunuo 3:20*).

Po pote ulipo katika maisha wakati huu wa sasa, Mungu yupo karibu na wewe zaidi kuliko unavyofikiria. Anataka kumwaga mibaraka yake kwa familia yako, kwa kanisa lako, kwa jamii yako, na kwa ulimwengu wako. Ungana nasi sasa katika kuomba kwa ajili ya uamsho wa kiroho kupitia kwa Roho Mtakatifu!

Mambo ya kawaida ya maombi katika siku kumi za maombi

Miongozo ya Maombi ya Kila Siku

Tumetoa mwongozo wa maombi ya kila siku katika siku hizi kumi. Mwongozo wa kila siku husika hujumuisha aya ya Biblia itakayotumika katika kuomba, somo la kasha, aya

za Biblia za kutumia katika kuomba, mapendekezo ya maombi, na mapendekezo ya nyimbo. Tunapendekeza kuwa ikiwezekana utoe nakala ya kurasa za miongozo ya kila siku ili kila mshiriki aweze kuwa na nakala yake apate kufuatisha katika ule muda wa maombi.

Makanisa ulimwenguni yataungana katika kuomba kuhusu mada ya kila siku. Ungana nao katika kuomba kupitia katika aya na mahitaji yaliyoletwa, lakini usihisi kwamba unapaswa kupitia kwa haraka katika orodha yote ya mahitaji ya maombi. Mnaweza kugawanyika katika vikundi vidogo na kila kikundi kikaombea sehemu ya orodha ya mahitaji yenu ya kuombea

Pia tumejumuisha ukurasa unaoitwa Maombi ya Kanisa la Kiulimwengu. Ni muhimu kuomba pamoja kwa ajili ya familia ya kanisa letu la kiulimwengu, lakini unaweza kutumia muda zaidi katika kuombea mahitaji ya eneo mahalia ikiwa kundi lako linajumuisha wageni kutoka kwenye jamii. Ombo kuhusu namna unavyoweza kuwakaribisha wageni kwa ubora Zaidi na kuwafanya wajisikie kuwa ni sehemu ya kundi hilo.

Muda unaopendekezwa kwa ajili ya kila Kipengele cha Maombi

Fanya muda wenu wa maombi kuwa wa kawaida na rahisi ili kundi liweze kuelekeza mawazo yao katika kuomba. Muda utakaotumika katika kila kipengele utatofautiana. Mwongozo ufuatao ni mapendekezo tu:

- **Kukaribisha/Utangulizi** – dakika 2 hadi 5
- **Usomaji wa “Ushuhuda” (mwongozo wa maombi wa kila siku)** – dakika 5
- **Kuomba Kupitia mafungu katika “Kuomba Neno la Mungu” (mwongozo wa maombi wa kila siku)** – dakika 10 hadi 15
- **Kuombea mahitaji katika “Mapendekezo zaidi ya Maombi” (mwongozo wa maombi wa kila siku)** – dakika 30
- **Kushukuru kwa nyimbo na sifa** – dakika 5 – 10

Kuombea Wengine

Hamasisha kila mtu kuombea watu watano hadi saba ambaa Mungu ameweka katika maisha yao. Wanaweza kuwa ndugu, marafiki, wafanyakazi wenza, majirani, au watu wanaofahamiana nao. Wahamasishhe kumwomba Roho Mtakatifu awaongoze katika

kuchagua majina haya na kuwafikia watu hao katika siku hizi kumi za maombi. Unaweza kutoa kadi au vikaratasi ambavyo watu watatumia kuandika majina watakayokuwa wakiombea.

Huduma za Sabato katika Kipindi cha Siku Kumi za Maombi

Maombi na yalenge katika kitu mahususi, na ni vyema kushiriki pamoja shuhuda mbali mbali za maombi yaliyojibiwa katika huduma siku ya Sabato kanisani kwa Sabato zote mbili. Kuwa mbunifu - kuna namna nyingi za kushiriki pamoja na familia ya kanisa mambo yanayotokea katika mikutano ya maombi ya kila siku.

Sherehe za Sabato ya Kuhitimisha

Sabato ya mwisho inapaswa kutayarishwa kwa namna itakayokuwa ni muda wa furaha kuu kwa yale yote Mungu aliyotenda katika siku hizi kumi. Tenga muda wa kutosha kwa ajili ya shuhuda za maombi yaliyojibiwa, kwa ajili ya mafundisho ya kibiblia/mahubiri juu ya maombi, na kwa ajili ya nyimbo. Ongoza kusanyiko katika muda wa maombi ili kwamba hata wale ambao hawakuhudhuria mikutano ya kila siku, wapate uzoefu wa furaha ya kuomba pamoja na wengine. Tafadhali tazama mwongozo wa Sherehe za Sabato kwa mawazo zaidi.

Kufuatilia kipindi hiki cha maombi ya siku kumi

Omba kuhusu namna Mungu anavyotaka kanisa au kikundi chako kuendeleza kile Alichanzisha katika kipindi cha Siku Kumi za Maombi. Pengine mtaendelea kukutana kila juma kwa ajili ya maombi. Au pengine Mungu anataka muanze huduma mpya ndani ya kanisa lenu au katika kuifikia jamii. Muwe tayari na kumfuata Mungu kule anapowaelekeza. Hakika mtashangazwa kadiri mnavyotembea pamoja naye. Ukurasa wa Changamoto ya Kuwafikia Wengine umejaa mawazo ya huduma.

Shuhuda

Tafadhali shiriki visa vinavyoonesha jinsi Mungu alivyatenda kazi katika Siku Kumi za Maombi! Visa vyako vitakuwa msaada na hamasa kwa wengine wengi. Shuhuda zinaweza kutumwa kwa: stories@ministerialassociation.org au kutumwa mtandaoni kwenye tovuti hii: www.tendaysofprayer.org.

Vielekezi vya kuunganika katika maombi

Kubalianeni

Mtu anapoombea hitaji fulani kwa Mungu, hakikisha kuwa wengine pia wanaombea hitaji hilo hilo na kukubaliana – kufanya hivi kuna nguvu! Usifikiri kwamba kwa sababu mtu mmoja ameomba kuhusu hitaji hilo, hakuna haja ya mwingine kuliombea. "Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni" (*Mathayo 18:19*). Inatia moyo kiasi gani kuinuliwa katika maombi!

Kudai Ahadi za Mungu

Hamasisha kikundi kudai ahadi za Mungu kadiri wanavyoomba. Ni rahisi sana kujielekeza katika matatizo yetu. Lakini tunapodai ahadi za Mungu, tunaongeza imani yetu na kujikumbusha kwamba hakuna kinachoshindikana kwa Mungu. Ahadi hizo hutusaidia kuondoa macho yetu kwenye madhaifu na magumu tunayokabiliana nayo, na kuyaelekeza kwa Yesu. Tunaweza kupata ahadi za Biblia za kudai kwa kila udhaifu na kila pambano. Himiza watu kutafuta ahadi nyingi zaidi iwezekanavyo na kuziandika ili waweze kuzidai wakati ujao.

Kufunga

Alika wale wanaoungana nawe katika Siku Kumi za Maombi kufikiria aina ya kufunga watakayoshiriki, kwa mfano kufunga na kuacha kutazama televisheni, kusikiliza muziki wa kidunia, kutazama filamu, kuingia mtandaoni, kula vitu vitamu vitamu kama vile pipi, au aina nyingine ya vyakula ambavyo ni vigumu kumeng'enywa. Tumia muda wa ziada katika kuomba na kujifunza Biblia, ukimwomba Mungu akusaidie wewe na kusanyiko lako kudumu kikamilifu zaidi katika Kristo. Kwa kuchagua mlo mwelesi, tunaruhusu akili zetu kuwa sikivu zaidi kwa sauti ya Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu

Hakikisha unamwomba Roho Mtakatifu akuonyeshe jambo la kuombea katika maisha ya mtu au katika hali fulani. Biblia inatuambia kwamba hatufahamu tuombe nini, na kwamba Roho Mtakatifu ndiye anayetuombea.

"Hatupaswi kuomba tu kwa jina la Kristo, bali kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hii huelezea maana halisi tunaposema kuwa Roho "*hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa*." (*Warumi 8:26*). Mungu hufurahia kujibu ombi kama hilo. Tunapoomba kwa dhati na kwa nguvu tunaomba kwa jina la Kristo, katika nguvu hiyo kuna ahadi kutoka

kwa Mungu kwamba anakaribia kujibu maombi yetu kama tunavyosoma kuwa, "Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaoombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu" (Waefeso 3:20)" (*Christ Object Lessons*, uk. 147, *msisitizo umeongezewa*).

Kutunza Taarifa ya Maombi

Kutunza daftari la kumbukumbu ya maombi kwenye kipindi chote cha Siku Kumi za Maombi kunaweza kuwa njia bora ya washiriki kuhifadhi moyoni wazo kuu la maombi ya kila siku, kufanya maagano thabiti na Mungu, na kutambua mibaraka yake kwao. Kuorodhesha maombi yetu na kutunza kumbukumbu ya majibu ya Mungu ni njia iliyothibitishwa ya kutia moyo.

Ikiwa utapenda, unaweza kutenga muda pale mmapokutanika kwa ajili ya maombi, ili watu wapate kuandika mwitikio wao kwa Mungu kwenye shajara zao binafsi za maombi. Au unaweza kutunza shajara ya kikundi ya maombi na majibu yake - linaweza kuwa ni daftari, au bango kubwa, au unaweza kutunzia mtandaoni. Inafurahisha na pia inajenga imani unapotazama nyuma na kuona jinsi Mungu alivyojibu maombi!

Kicho

Himiza na kujenga mtazamo wa kicho na unyenyekevu. Tunakaribia chumba chenye kitit cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu. Hebu túsitumie muda huu wa maombi vibaya kwa mkao wetu na kwa mwenendo wetu na hata katika mazungumzo yetu. Hata hivyo, siyo lazima kila mmoja apige magoti muda wote. Unahitaji watu wawe huru kwa saa moja, hivyo wahamasishe watu kupiga magoti au kukaa au kusimama kadiri Mungu atakavyokuongoza na jinsi wanavyokuwa huru zaidi.

Maombi kwa Sentensi

Maombi yanapaswa kuwa mafupi, na yaelekezwe moja kwa moja kwenye hitaji. Kufanya hivi kutawapatia wengine pia fursa ya kuomba. Jaribu kufupisha maombi yako yawe ni ya sentensi chache. Kila mmoja anaweza kuomba mara kadhaa. Maombi mafupi yatafanya kipindi cha maombi kiwe cha kufurahisha na siyo kinachochosha na hivyo kumruhusu Roho Mtakatifu aguse kundi zima akiwaonesha namna ya kuomba. Siyo lazima kuanza na kumaliza ombi fupi la sentensi kwa maneno kama "Mungu wetu mpPENDWA" na "Amina." Ni mawasiliano endelevu na Mungu.

Ukimya

Wewe kama kiongozi usitawale kipindi cha maombi. Lengo kubwa ni kuwawezesha wengine kuomba. Kipindi cha ukimya kina thamani kubwa ajabu, kwani humpa Mungu muda wa kuzungumza na mioyo yetu. Mruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi kwa kumpa kila mmoja muda wa kutosha wa kuomba.

Kuimba

Nyimbo za hapa na pale kutoka kwa vikundi zikiunganishwa kwenye maombi, huongeza uzuri katika mukutano wa maombi. Nyimbo zilizopendekezwa zimeorodheshwa mwisho wa kila ukurasa wa wazo la siku. Siyo lazima kutumia nyimbo zote - haya ni mapendekezo tu. Kuimba pia ni njia nzuri ya kuhama kutoka kwenye kipindi kimoja kwenda kwenye kipindi kingine.

Kukusanya Mahitaji ya Kuombea

Usiulizie na kukusanya mahitaji ya kuombea kutoka kwenye kikundi. Badala yake, waambie watu wataje mahitaji yao wakati wanapoomba na kuwahimiza wengine kuijunga wakikubaliana nayo kwa kuungana katika maombi kimya kimya. Sababu kubwa ni Muda! Kuzungumza kuhusu mahitaji ya kila mmoja kunaweza kutumia muda mwingi wa maombi. Shetani anafurahi akiweza kutudumisha katika kuzungumzia tatizo badala ya kuomba kwa ajili ya tatizo hilo. Wanakikundi wanaweza kuanza kushauriana na kupendekeza ufumbuzi. Uwezo unatoka kwa Mungu! Kadiri tunavyoongeza maombi ndivyo anavyoachia uwezo wake.

Muda wako wa kila siku

Ni wa muhimu sana! Hakikisha wewe kama kiongozi unatumia muda wako mwingi miguuni pa Yesu, ukizungumza naye na kusoma Neno lake. Ikiwa utafanya kumfahamu Mungu kuwa kipaumbele chako katika maisha, utafunguliwa uzoefu ulio mzuri wa ajabu. "Kutoka katika sehemu ya siri ya maombi ilitoka Nguvu ya ajabu iliyotikisha dunia na kuleta Matengenezo Makuu. Hapo, kwa utulivu mtakatifu, watumishi wa Bwana waliweka miguu yao katika mwamba wa ahadi zake" (*The Great Controversy*, uk. 210). Kiongozi anapoomba, Mungu hushughulika na mioyo!

Utangulizi

Karibu katika Siku Kumi za Maombi 2021! Tunaamini kuwa, katika maombi ndipo mahali uamsho unapozaliwa. Mungu ametenda miujiza minge katika miaka iliyopita kadiri tulivyokuwa tukimtafuta kwa kuomba na kufunga. Roho Mtakatifu amewezesha uamsho, mabadiliko, hisia za uinjilisti zilizojengwa upya, makanisa yaliyoamshwa, na mahusiano yaliyoponywa. Hapa kuna baadhi ya shuhuda katika miaka iliyopita:

Katika kipindi cha Siku Kumi za Maombi nilitoa maombi mawili:

1. *Binti yangu aweze kufunguliwa kutoka katika kifungo cha uraibu na mume wangu ajitoe kwa Bwana.*

[Mwaka uliofuata] Nilikuwa nikimsifu Mungu kwa uwezo wa binti yangu nikisema kwamba alikua 'safi' kutoka katika uraibu wa 'methamphetamine kwa muda wa miezi ninane sasa,' si mtu asiye na makazi tena, na anayefanya kazi muda wote. Mume wangu alibatizwa tena na alihudhuria pamoja nami katika Siku Kumi za Maombi mwaka huu. Sifa zote ziwe ni kwa Bwana, Baba yetu, kupitia kwa Yesu Kristo. (N.H.)

Kama kanisa, tulianza kuomba kwa ajili ya mvua kwani nchi yetu ilikabiliwa na ukame. Lilikuwa ni janga kubwa na kila mmoja wetu alikuwa na hofu, lakini ninataka kumshukuru Mungu kwamba baada ya siku tatu, alijibu maombi yetu. Sasa mvua zinanyesha kila siku. (L.M.)

Kupitia katika maombi wagonjwa waliponywa, wanafamilia waliotengana waliungana tena, tumaini lilikuwepo hata katika kifo cha wapendwa, na watu walitoa upya maisha yao kwa Mungu. Tunamtumikia Mungu aliye hai! Tunasubiri kwa hamu kuona kile alichotuandalia mwaka huu. (Dereck)

Je, sauti ya Mungu imekuwa ikikuita kufanya uamsho? Biblia imejaa ahadi kwa ajili yako:

"Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao" (2 Nyakati 7:14).

"Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote" (Yeremia 29:13).

"Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliita jina la Bwana ataponywa" (Yoeli 2:32).

"Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi" (Yakobo 4:8).

"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlangano, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami" (Ufunuo 3:20).

Po pote ulipo katika maisha sasa, Mungu yupo karibu zaidi kuliko unavyofikiri. Anataka kumwaga mibaraka yake kwa familia yako, kanisa lako, jamii yako, na ulimwengu wako. Ungana nasi sasa katika kuomba kwa ajili ya uamsho wa kiroho kupitia kwa Roho Mtakatifu!

Mada yetu ya Maombi: Kutafuta Uamsho

Mwaka huu tunakualika kutafuta uamsho kupitia kwenye nguvu ya Roho Mtakatifu katika Siku Kumi hizi za Maombi. Kadiri unavyoomba, dai ahadi ya Mungu kwa Zerubabeli na kuifanya kama ya kwako: "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi" (Zakaria 4:6). Kwa maneno mengine, "'Unachopanga hakitafanikiwa, iwe ni kwa nguvu za jeshi au ni kwa nguvu ya kibinadamu; badala yake, Roho Wangu atakikamilisha!' Mimi, Bwana mwenye Nguvu, ninaahidi hili" (imetafsiriwa na Helmut Haubeil kutoka Ujerumani – toleo la *Hoffnung fuer Alle*).

Mungu anataka kufanya mambo ya ajabu katika maisha yetu na makanisa yetu leo. Mpango wake unazidi uwezo wetu, ni kwa muunganiko wa kudumu wa maombi pamoja naye, ndipo tunapoweza kukamilisha kazi yaliyotuandalia. Anatusihi, "Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua" (Yeremia 33:3).

Ungana nasi katika kuombea uamsho na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kulioahidiwa. Utafute ufalme wa Mungu kwanza, na utazame anavyofungua madirisha ya Mbinguni!

Mwongozo unaopendekezwa wakati wa maombi

- Jitahidi kufanya maombi yawe mafupi – sentensi moja au mbili kuhusu mada husika. Kisha waacie wengine. Unaweza kuomba mara nyingi kadiri unavyojisikia, kwa namna ile ile unayozungumza katika mazungumzo.
- Msigope kuwa kimya, kwani kuwa kimya kunampatia kila mmoja muda wa kumsikiliza Roho Mtakatifu.

- Kuimba nyimbo pamoja kadiri Roho Mtakatifu atakavyowaongoza ni mbaraka mkubwa. Hamhitaji kinanda ili kuwaongoza; kuimba bila ala ya mziki ni sawa pia.
- Badala ya kutumia muda wa thamani wa maombi ukizungumza kuhusu mahitaji yako ya kuombea, bali yaombee tu. Kisha wengine pia wanaweza kuombea mahitaji yako na kudai ahadi kwa ajili ya mahitaji yako.

Kudai Ahadi

Ni faida kwetu kudai ahadi hizo katika maombi. Maagizo yote ya Mungu na mashauri yake pia ni ahadi. Hawezi kudai kutoka kwetu jambo fulani ambalo hatuwezi kufanya kwa uweza wake.

Tunapoomba, ni rahisi kujielekeza katika mahitaji yetu, magumu yetu, changamoto zetu - na hasa kulalamika na kulaumu kuhusu hali tuliyo nayo. Hili silo kusudi la maombi. Kusudi kubwa la maombi ni kuimarisha imani yetu. Ndiyo maana tunakuhimiza kudai ahadi za Mungu katika muda wako wa maombi. Hamisha macho yako kutoka katika mahitaji yako na changamoto zako na kuyaelekeza kwa Yesu Kristo. Ni kwa kumwangalia yeye pekee ndipo tunapobadilishwa na kuchukua sura yake.

Ellen White anatutia nguvu kwamba: "Kila ahadi katika Neno la Mungu ni kwa ajili yetu. Katika maombi yako, wasilisha neno lililoahidiwa la Yehova uidai kwa imani ahadi zake. Neno lake linatupatia uhakika kwamba ukiomba kwa imani, utapokea mibaraka yote ya kiroho. Endelea kuomba nawe utapata zaidi ya yale uyaombayo au uyawazayo." (*In Heavenly Places*, uk. 71).

Ni kwa namna gani unaweza kudai hizo ahadi za Mungu? Kwa mfano, unapoomba kwa ajili ya amani, unaweza kudai Yohana 14:27 na kusema kuwa, "Bwana umetuambia katika Maandiko yako kwamba 'Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga.' Ninakuomba unipatie amani uliyoahidi kutuachia." Kisha mshukuru Bwana kwamba atakupatia hiyo amani hata kama haujisikii kuwa na amani wakati huo.

Kufunga

Tunakuhamasisha kufanya Mfungo kama ule wa Danieli katika Siku hizi Kumi. Kuanza mwaka kwa maombi ya kufunga ni njia bora ya kuweka wakfu maisha yetu kwa Mungu kwa mwaka unaoanza. Ellen White anatuambia, "Sasa na kuendelea hata mwisho wa wakati watu wa Mungu wanapaswa kuwa na bidii zaidi, kuwa macho zaidi,

kutokuamini hekima yao wenyewe, lakini kuamini hekima ya kiongozi wao, ambaye ni Yesu. Wanapaswa kutenga siku kwa ajili ya kufunga na kuomba. Kujitenga kabisa na chakula kunaweza kusiwe lazima, lakini wanapaswa kula vyakula rahisi zaidi" (*Counsels on Diet and Foods*, uk. 188, 189).

Tunafahamu kuhusu Danieli, aliyekula matunda na mboga mboga kwa siku kumi. Sisi pia tunakuhamasisha kuwa na mlo rahisi sana katika siku hizi kumi. Mlo rahisi unaoweka kando sukari, vyakula viliyyotengenezwa kiwandani, na soda huweza kutufaidisha kwa ngazi tofauti. Kwanza, kula chakula rahisi humaanisha muda mchache huhitajika kuandaa chakula na muda mwangi kutumika pamoja na Bwana. Pili, chakula chetu kinapokuwa rahisi zaidi, ndivyo inavyokuwa rahisi kwa matumbo yetu kukimeng'enya, na akili zetu zitakua wazi zaidi. Sote tunafahamu kwamba sukari hufunika sehemu inayotawala kuwaza kwetu. Kama tunataka akili zilizo wazi zaidi ili kuisikia sauti ya Mungu, na kama tunataka kuwa karibu zaidi na Mungi, tunahitaji kuhakikisha kwamba chakula chetu hakiturudishi nyuma.

Kufunga si kujitenga tu na chakula. Tunakuhamasisha pia kufunga kutazama televisheni, filamu, michezo ya kompyuta, na hata Facebook na YouTube. Wakati mwagine vitu visivyo vibaya, kama Facebook na YouTube, huweza kutuchukulia muda mwangi sana. Weka kando kila kinachowezekana ili uwe na muda mwangi wa kukaa na Bwana.

Kufunga siyo njia ya haraka ya kupata mibaraka kutoka kwa Mungu. Kufunga ni kujinyenyekeza wenyewe ili kwamba Mungu aweze kufanya kazi ndani yetu na kupitia kwetu. Hebu na tusogee karibu naye kupitia maombi ya kufunga, naye atasogea karibu Zaidi nasi.

Roho Mtakatifu

Hakikisha unamuomba Roho Mtakatifu akuonyeshe unachopaswa kuombea katika maisha ya mtu au katika hali fulani. Biblia inatuambia kwamba hatufahamu namna ya kuomba na kwamba Roho Mtakatifu ndiye anayetuumbea.

"Hatupaswi kuomba tu kwa jina la Kristo, lakini kwa msukumo wa Roho Mtakatifu. Hii huelezea maana ya maneno kwamba Roho "hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa." (Warumi 8:26). Ombi kama hilo Mungu hufurahia kulijibu. Tunapoomba kwa dhati na kwa nguvu tunaomba kwa jina la Kristo, katika nguvu hiyo kuna ahadi kutoka kwa Mungu kwamba anakaribia kujibu maombi yetu 'zaidi ya tuyaoombayo au tuyawazayo' (Waefeso 3:20" (*Christ Object Lessons*, uk. 147).

Imani

Tunasoma katika Roho ya Unabii kwamba "maombi na imani vitafanya kile ambacho hakuna nguvu duniani inachowenza kufanya" (*The Ministry of Healing*, uk. 509). Pia tunaambiwa kwamba "ahadi yo yote aliyoahidi, tunaweza kuiomba; kasha tunapaswa kuamini kwamba tumeipokea, na kurudisha shukrani kwa Mungu kwamba tumepokea" (*Education*, uk. 258). Hivyo jenga tabia ya kumshukuru Mungu kabla kwa imani kwa kile atakachoenda kutenda na namna atakavyoenda kujibu maombi yako.

Ombea Wengine

Katika siku hizi kumi tunakuhamasisha kuombea watu ambao Mungu amewaweka katika maisha yako kwa namna ya pekee. Chagua watu watano hadi saba – wanaweza kuwa ndugu, marafiki, wafanyakazi wenzako, majirani, au hata watu unaowafahamu tu. Tenga muda kumuuliza Mungu kuwa, angependa umuombee nani. Mwombe pia akupatie mzigo halisi wa watu hawa. Andika majina yao kwenye karatasi na uitunze sehemu salama, kama kwenye Biblia yako. Kuna jambo lenye nguvu katika kuyaandika majina hayo, na utashangazwa namna Mungu anavyofanya kazi katika kujibu maombi yako!

USIKU WA MAOMBI:

Fikiria kuandaa huduma ya maombi ya usiku kama sehemu ya Siku Kumi za Maombi. Kwa mfano, unaweza kuanza saa 12 jioni na kumaliza saa 12 asubuhi. Chagua ratiba utakayofaa kwa kundi lako.

Kwa nini kuwa na Usiku wa Maombi?

Hakuna chochote “kitakatifu” katika kukesha na kuomba usiku kucha. Hata hivyo, ni kweli kwamba usiku unaweza kuwa ni wakati wa pekee ambao watu hawana mambo mengi au haraka. Tunaamini kwamba lengo lako halipaswi kuwa kukaa usiku kucha, bali ni kuomba sana kadiri inavyohitajika hadi utakapokuwa umeombea vitu vyote unavyohisi kwamba Mungu anataka uviombee.

Tunapendekeza kwamba baadhi ya watu waongoze usiku huo. Hakikisha kunakuwa na mapumziko. Kama kiongozi, unaweza kuona hali ilivyo na kufahamu wakati mapumziko yanapohitajika na wakati utakapoona inafaa kuhamia katika kipengele kinachofuata cha maombi. Unaweza pia kuingiza usomaji wa vifungu vya Biblia katika muda wako wa maombi. Unaweza kufanya mambo yote yaliyopendekezwa au baadhi yake, inategemea kile kilicho bora kwa kikundi chako. Kuwa huru kubadilisha mtiririko kadiri utakavyoona inafaa.

Mapendekezo ya Mpangilio wa Usiku wa Maombi

- *Anza kwa kipindi cha sifa.* Msifu Mungu katika maombi yako na pia kupitia nyimbo.
- *Tumia muda kwa ajili ya kuungama,* ukihakikisha kwamba hakuna kinachomzia Mungu kusikia maombi yako. Wapatie watu muda wa kuungama binafsi na weka muda wa kuungama kwa pamoja. Hamasisha watu kuungama dhambi za binafsi wakiwa pekee yao na kuungama dhambi za wazi kwa uwazi. Katika Danieli 9:1-19 tunasoma kumhusu Danieli, aliyeomba na kuungama kwa wazi dhambi za watu wa Mungu.
- *Ombea mahitaji ya watu walio katika mkutano huo wa maombi.* Watu wengi wanaumia au wana uhitaji wa maombi, au wanamfahamu mtu mwenye uhitaji wa maombi. Tengeneza duara, weka kitu katikati, na alike wale wenye maombi maalumu waje mmoja baada ya mwagine na kushiriki maombi yao. Kasha

kusanyikeni kumzunguka mtu huyu na waruhusu watu wawili au watatu kuomba kwa ajili ya mahitaji mahususi ya mtu huyo na kudai ahadi za Mungu.

- *Gawanya kundi katika vikundi viwili.* Waruhusu wanawake kuomba katika chumba kimoja (wakiwa na kiongozi wa kike) na wanaume katika chumba kingine (wakiwa na kiongozi wa kiume). Mahitaji mengi binafsi hayawezi na hayapaswi kushirikishwa na kila mtu. Ni rahisi zaidi kushiriki pamoja na wale wa jinsia moja.
- *Baada ya kurudi pamoja, ombea mahitaji ya jamii na kanisa lenu.* Pia tumia muda kwa ajili ya **maombi ya kanisa la kiulimwengu** (yaliyoorodheshwa katika ukurasa wa maombi ya kanisa la kiulimwengu). Usihisi kwamba unapaswa kuharakisha kuimaliza orodha nzima. Unaweza kugawanyika katika makundi madogo na kuwapatia kila kundi sehemu ya orodha hiyo.
- *Ombea orodha ya watu watano hadi saba* uliokuwa ukiwaombea katika siku hizi kumi
- *Chagua kifungu cha Biblia na kuombea.*
- *Funga muda wa maombi kwa kipindi kingine cha kusifu na kushukuru.*

Changamoto za Kuwafikia watu walio nje katika Siku Kumi za Maombi

Yesu hatuiti kwa ajili ya kuomba tu bali pia kuhudumia mahitaji ya wale wanaotuzunguka. "Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia" (Mathayo 25:35, 36).

Katika kitabu cha *Huduma ya Uponyaji* (*The Ministry of Healing*) tunasoma kuwa, "Tunapaswa kuishi maisha yenyeye sura mbili – maisha ya mawazo na matendo, na maisha ya maombi ya kimya na kazi inayofanywa kwa juhudhi" (uk. 512). Tumepokea upendo mwingi sana kutoka kwa Mwokozi wetu; na tuna fursa ya kushiriki upendo huo na marafiki, majirani, hata watu tusiowafahamu wenyewe uhitaji.

Muulize Mungu katika maombi namna bora ya kuwafikia wengine katika Siku hizi Kumi za Maombi. Unapokuwa ukifanya kazi ya kupanga kila kitu, epuka kuruhusu shughuli hizo kukufanya ushindwe kuomba. "Jithada binafsi kwa ajili ya wengine zipanapaswa kwanza kutanguliwa na maombi mengi ya siri; kwani hekima kubwa inahitajika ili kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na watu, wasiliana na Kristo. Pata maandalizi ya kuhudumia watu kutoka katika kiti cha enzi cha neema ya kimbingu." (*Maombi*, uk. 313).

Hapa kuna baadhi ya njia unazoweza kutumia kusaidia wengine. Chagua njia yo yote utakayoona inakidhi mahitaji ya wale unaokwenda kuwahudumia, na jisikie huru kuongeza mawazo yako.

- Mpikie mgonjwa chakula.
- Mkaribishe jirani/mfanyakazi mwenzako kwenye kusanyiko la kijamii.
- Mpatie chakula mtu asiye na makazi.
- Tafuta mzee mmoja. Mtembelee kila siku na umsaidie kazi, kama vile kumnunulia mahitaji, kumpikia, au kumsaidia kazi za bustani, n.k.
- Oka mkate na ushiriki huo mkate na jirani.
- Saidia kwenye miradi katika maeneo yanayokuzunguka.
- Jitolee kukaa na mgonjwa au mtu asiyejiweza ili wale wanaomhudumia waweze kufanya shughuli zingine.

- Jitambulisse kwa jirani mpya aliyehamia maeneo yenu na kumpeleke chakula. Mfanye ajisikie kukaribishwa katika maeneo hayo.
- Nunua mahitaji ya jikoni na upelekee familia yenyе uhitaji.
- Toa msaada miwani yako ya zamani.
- Jitolee kutoa masomo ya Biblia
- Tembelea sehemu za kutunzia watu wenyе uhitaji na kuwafariji.
- Mpatie mwanafunzi fedha ya "chakula."
- Kusanya nguo kwa ajili ya wahitaji. Unaweza kuanzisha kabati la nguo kanisani kwako kwa ajili ya kushirki na wale walio na uhitaji.
- Toa msaada kompyuta yako au vifaa vingine vya kielektroniki usiyoyotumia.
- Toa msaada gari lako lililotumika.
- Andaa "Tamasha la Kupima Afya."
- Tuma kadi kwa mtu aliyefungiwa ndani.
- Andaa mfululizo wa mambo ya uinjilisti.
- Mpatie mtu kitabu unachodhani angekipenda.
- Wapigie simu jirani zako na kuwajulia hali.
- Gawa vijarida na vijuzuu kwa watu. Vinapatiakana kwenye tovuti ifuatayo hapa:
www.glowonline.org/glow
- Mwalike mtu kumpokea Yesu.
- Endesha darasa la mapishi.
- Fanya "Mradi wa machapisho 28." Katika Juma la kwanza, gawa kitabu kimoja. Juma la pili, gawa vitabu viwili. Juma la tatu, gawa vitabu vitatu. Endelea hadi utakapogawa vitabu vyote 28.
- Mpelekee chakula mtu aliyepoteza (aliyefiwa na) mpendwa wake.
- Mtembelee mtu hospitali ili kumtia moyo au kumsaidia kwa namna moja au nyingine.
- Msomee mzee kitabu.
- Tembelea makazi ya watoto yatima pampja na wanaoishi katika mazingira magumu na toa msaada kwa wafanyakazi wa hapo.
- Anza kundi la kushona/kufuma ili kutengeneza nguo kwa ajili ya wahitaji.
- Msomee Biblia kwa sauti mtu asiyeo na asiyeweza kusoma.
- Endesha usiku wa vijana nyumbani kwako.
- Toa makazi kwa watu walionyanyaswa.
- Gawa baadhi ya vitabu kwenye makazi ya watoto.
- Panga na kusimamia siku ya kufurahi kwa ajili ya watoto na wenyе mahitaji maalumu pamoja na familia zao.

- Andaa siku ya kufanya usafi katika jamii.
- Anzisha chama cha afya katika kanisa lako. Aliku marafiki na majirani.
- Muulize mtu kama angependa kuungana na wewe kutazama mkanda wenye ujumbe wa kiroho. Kadiri mnavyotazama pamoja, omba kwamba Roho Mtakatifu anene na moyo wa mtu huyo.
- Buni mradi wako mwenyewe.

Kwa vitendea kazi zaidi juu ya ushuhudiaji, tembelea tovuti ifuatayao:

www.revivalandreformation.org/resources/witnessing.

Ahadi za Kudai kwenye Maombi

Ahadi za Roho Mtakatifu

“Mwombeni Bwana mvua wakati wa masika, naam, Bwana afanyaye umeme, naye atawapa manyunu ya mvua, kila mtu atapewa nyasi kondeni.” Zakaria 10:1

“Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?” Luka 11:13

“Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia... Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.” Yohana 14:26; 16:8

“Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.” Yohana 14:12 – 14

“Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi.” Zakaria 4:6

Ahadi kwamba Mungu Hujibu Maombi

“Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.” Yohana 15:7

“Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.” Waebrania 4:16

“Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Marko 11:24

“Ukaniite siku ya mateso; Nitakuokoa, na wewe utanitokuza.” Zaburi 50:15

“Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni.” Mathayo 18:19

"Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea." Mathayo 21:22

"Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya." Yohana 14:13, 14

"Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote. Amin, amin, nawaambia, Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu." Yohana 16:23, 24

"Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba." 1 Yohana 5:14, 15

Ahadi kuhusu Nguvu ya Mungu

"Kuna neno gani lililo gumu la kumshinda Bwana? Kwa muhula wake nitakurudia, wakati huu huu mwakani, na Sara atapata mwana wa kiume." Mwanzo 18:14

"Bwana atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya." Kutoka 14:14

"Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana yote yavezekana kwa Mungu." Marko 10:27

"Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya." 1 Wathesalonike 5:24

"Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuulika." Ayubu 42:2

"Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?" Warumi 8:31, 32

"Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalifikiliza?" Hesabu 23:19

"Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki; akili zake hazichunguziki. Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo. Hata vijana watazimia na kuchoka, na wanaume vijana wataanguka; bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia." Isaya 40:28 - 31

Ahadi za Uongozi wa Mungu

“Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.” Yoshua 1:9

“Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanya hayo niliyokuambia.” Mwanzo 28:15

“Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea.” Kutoka 23:20

“Lakini huko, kama mkimtafuta Bwana, Mungu wako, utampata, ukimtafuta kwa moyo wako wote, na roho yako yote.” Torati 4:29

“Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua.” Yeremia 33:3

“Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa; Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja; Kwa kuwa kinywa cha Bwana kimenena haya.” Isaya 40:4, 5

“Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; Nitakushauri, jicho langu likikutazama.” Zaburi 32:8

“Naye Bwana, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike.” Torati 31:8

“Ni nani amchaye Bwana? Atamfundisha katika njia anayoichagua.” Zaburi 25:12

“Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako.” Mithali 3:5, 6

“Na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.” Isaya 58:10, 11

“Nao watatoka nje na kuitazama mizoga ya watu walioniasi; maana funza wao hatakufa, wala moto wao hautazimika nao watakuwa chukizo machoni pa wote wenye mwili.” Isaya 65:24

Ahadi za Moyo Uliobadilishwa

“Nami nitawapa moyo, wanijue ya kuwa mimi ni Bwana; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao; kwa maana watanirudia kwa moyo wao wote.” Yeremia 24:7

“Bwana, Mungu wako, atautahiri moyo wako, na moyo wa uzao wako, ili umpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, upate kuwa hai.” Torati 30:6

“Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama.” Ezekieli 36:26

“Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba ye ye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu;” Wafilipi 1:6

“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipyta; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.” 1 Wakorintho 5:17

“Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.” Wagatalia 2:20

“Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya.” 1 Wathesalonike 5:23, 24

Ahadi za Msamaha

“Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.” 1 Nyakati 7:14

“Kwa maana Wewe, Bwana, U mwema, Umekuwa tayari kusamehe, Na mwingi wa fadhili, Kwa watu wote wakuitao.” Zaburi 86:5

"Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu." Marko 11:25

"Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi." Waefeso 4:32

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 1:9

"Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu." Isaya 1:18

"Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako." Isaya 43:25

"Maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena." Yeremia 31:34

"Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake." Waefeso 1:7

Ahadi za Ushidi Dhidi ya Dhambi

"Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulmwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulmwengu, hiyo imani yetu." 1 Yohana 5:4

"Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda." Warumi 8:37

"Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo." 1 Wakorintho 15:57

"Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu." Isaya 41:10

"Zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu." Waefeso 6:16

"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." Wagalatia 2:20

"Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." Wafilipi 2:13

"Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili." Wagalatia 5:16

"Naye Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi. Amina." Warumi 16:20

"Wala msiiufuatisho namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu." Warumi 12:2

"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake." 1 Yohana 2:15

Ahadi za Uponyaji

"Akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika amri zake, mimi sitatia juu yako maradhi yo yote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." Kutoka 15:20

"Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba; Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako." Torati 33:25

"Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, Wala usizisahau fadhili zake zote. Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote, Aukomboa uhai wako na kaburi, Akutia taji ya fadhili na rehema, Aushibisha mema uzee wako, Ujana wako ukarejezwa kama tai." Zaburi 103:2 - 5

"Usiwe mwenye hekima machoni pako; Mche Bwana, ukajiepushe na uovu. Itakuwa afya mwilini pako, Na mafuta mifupani mwako." Mithali 3:7, 8

"Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona." Isaya 53:3-5

“Uniponye, Ee Bwana, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana wewe ndiwe uliye sifa zangu.” Yeremia 17:14

“Maana nitakurudishia afya, nami nitakuponya jeraha zako, asema Bwana, kwa sababu wamekuita, mwenye kutupwa, wakisema, Ni Sayuni, ambao hapana mtu autakaye.” Yeremia 30:17

“Tazama, nitauletea afya na kupona, nami nitawaponya; nami nitawafunulia wingi wa amani na kweli.” Yeremia 33:6

“Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini.” Malaki 4:2

“Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa.” Yakobo 5:14, 15

Ahadi kwa ajili ya Nguvu za Kufanya Mapenzi ya Mungu

“Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.” 2 Wakorintho 4:16-18

“Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.” Wagalatia 6:9

“Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.” Wafilipi 4:13

“Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.” Wafilipi 2:13

“Naye akaniambia, Neema yangu yakutosh; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu.” 2 Wakorintho 12:9

Ahadi Kuhusu Kuwa Mashahidi wa Mungu

"Msiogope wala msifanye hofu; je! Sikukuhubiri haya zamani na kuyaonyesha? Na ninyi ni mashahidi wangu. Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine." Isaya 44:8

"Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia." Isaya 60:1

"Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho." 2 Wakorintho 5:18

"Lakini Bwana akaniambia, Usiseme, Mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru." Yeremia 1:7

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." Matendo 1:8

"Bali ninyi ni mzaao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaangie katika nuru yake ya ajabu." 1 Petro 2:9

"Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu." 1 Petro 3:15

Sherehe ya Siku ya Sabato ya Mwisho

Buni Sabato ya Mwisho ya Siku Kumi za Maombi kwa ajili ya kusherehekeea wema wa Mungu na nguvu yake kuu. Shiriki namna ulivyopata uzoefu wa umwagwaji wa Roho Mtakatifu katika siku hizi kumi zilizopita. Sherehekeea kwa yale Mungu aliyotenda, anayotenda, na atakayotenda.

Mahitaji ya kusanyiko yanatofautiana, hivyo tafadhali fanya kazi pamoja na viongozi wa kanisa mahalia ili kueandaa mpango mahususi kwa ajili ya kanisa lako. Hapa kuna baadhi ya mambo ya kujumuisha katika ibada ya kanisa lako katika Sabato ya Mwisho.

Wazo Kuu:

Kutafuta Uamsho kutoka kwa Roho Mtakatifu

Fungu Elekezi:

“Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu,’ asema Bwana wa majeshi” (Zakaria 4:6).

Mapendeleko ya Nyimbo

Kazi yangu ikiisha, No. 177

Mchana Hauishi, No. 182

Kuwa na Yesu, No. 51

Tusimame Imara Mwambani, No. 68

Mapendeleko ya Hubiri

Mruhusu mchungaji, mzee wa kanisa, au kiongozi wa maombi kuhubiri somo fupi kuhusu uamsho kupitia kwa Roho Mtakatifu. Fikiria kutumia moja kati ya mafungu haya ya Biblia:

- Luka 11:9-13 (kuomba na kupokea Roho Mtakatifu)
- Matendo 2 (umwagwaji wa Roho Mtakatifu kwa Wakristo wa awali)
- Warumi 8 (kuishi kulingana na Roho Mtakatifu)

Wapatie nafasi washiriki wa Siku Kumi za Maombi kupokezana katika kutoa muhtasari wa dakika 1 au 2 kwa kila mwongozo wa maombi wa siku 10. Shiriki kichwa cha somo, fungu elekezi, na wazo kuu. (Andaa mapema ili muhtasari uwe ndani ya dakika 1-2. Kwa watu wengi, dakika moja ni maneno 125-150).

[AU]

Andaa vijana wa kuwasilisha mafungu ya Biblia, masomo, au mahubiri mafupi yanayohusiana na wazo kuu la uamsho kupitia kwa Roho Mtakatifu. Vijana wanaweza pia kusaidia katika muziki au kutoa shuhuda.

Mawazo mengine ya Programu:

Shuhuda za washiriki juu ya maombi yaliyojibwa
Muda wa maombi ya vikundi vidogo
Matangazo ya maombi na shughuli zijazo za huduma
Kisa cha watoto kuhusu maombi
Chaguzi za nyimbo maalumu

Mahitaji ya Kuombea ya Kanisa la Kiulimwengu

Angalizo kwa viongozi: Ifuatayo ni orodha ya mahitaji ya kuombea ambayo ni endelevu kwa kanisa la kilimwengu la Waadventista wa Sabato. Kwa sababu masuala ya kilingwengu na ya kanisa yanabadilika kwa kasi kubwa, tutatoa orodha ya nyongeza iliyoboreshwa ya mahitaji ya kuombea katika tovuti yetu kadiri muda unavyoenda. Unaweza kutembelea tovuti ya: www.tendaysofprayer.org kwa nyongeza ya mahitaji.

1. Tunaomba kwa ajili ya washiriki wa Kiadventista wanaopitia mateso au vifungo kwa sababu ya Imani yao.
2. Tunaomba kwa ajili ya uamsho wa kiroho kati ya vijana Waadventista wa Sabato wanaohudhuria vyuo vya kiserikali ulimwenguni. Hebu na wawe mabalozi mashuhuri wa Kristo.
3. Tunaomba kwa ajili ya asilimia 69 ya idadi ya watu duniani ambao hawajapokea habari za Yesu zisizo na mawaa.
4. Tunaomba kwa ajili ya watu milioni 62 katika miji 28 ambayo haijafikiwa Zaidi katika unioni ya zamani ya Kirusi (Divisheni ya Ulaya na Asia).
5. Tunaomba kwamba Mungu ainue wamisionari wenyewe hekima walio tayari kufanya kazi kati ya makundi 746 ya watu kwenye nchi 20 za Mashariki ya Kati.
6. Tunaomba kwa ajili ya mafuriko makuu ya Waadventista watakaomtumikia Mungu kwa kuwapenda wengine na kushiriki pamoja na watu kutoka katika tamaduni na dini nyingine.
7. Tafadhali inua wanafuzi wa-Waldensia wa wakati huu tulio nao, walio tayari kukutumikia katika maeneo magumu.
8. Tunaomba kwa ajili ya watu milioni 202 katika miji 41 ambayo haijafikiwa Zaidi katika Divisheni ya Asia-Pasifikasi waweze kumfahamu Yesu.
9. Tunaomba kwa ajili ya Idara ya Shule ya Sabato na Idara ya Huduma binafsi ya kila kanisa mahalia kadiri wanavyotafuta mpango wa Mungu na kuzifikia jamii zao kwa huduma za upendo, Kujifunza Biblia, na ushuhudiaji binafsi.
10. Tunaomba kwa ajili ya shirika la ADRA (Adventist Development and Relief Agency) kadiri wanavyokabiliana na kukidhi mahitaji mahususi duniani.
11. Tunaomba kwa ajili ya watu milioni 16 katika miji 6 ambayo haijafikiwa Zaidi ya Divisheni ya Kusini mwa Pasifikasi.
12. Tunaomba Roho Mtakatifu atusaidia kufahamu namna ya kuwafikia watu milioni 406 katika miji 105 ya Divisheni ya Kaskazini mwa Asia-Pasifikasi isiyofikiwa Zaidi.

13. Tafadhali bariki Huduma za Chaplensia za Kiadventista kadiri zinavyosimamia chaplensia na washiriki wenyewe shauku katika kuhudumia wale walio katika magereza.
14. Bwana, tunakumbuka waalimu wetu wa Shule ya Sabato. Tafadhali wasaidie kufahamu kazi zao zilizo za muhimu kwa watoto wetu.
15. Bwana, tunatafuta uongozi wako katika Vituo vingi vya Vivutio, programu za afya na familia, na klabu za Watafuta Njia duniani.
16. Tunaomba kwamba utusaidie kuwapenda na kuwatunza waumini wapya.
17. Bwana, tafadhali tuonyeshe namna ya kutuma machapisho yaliyojazwa kweli (yaliyochapishwa na kielektroniki) katika jamii zetu. Tunaomba kwamba watu kuyasoma na Roho Mtakatifu awaonyeshe kweli ya Biblia.
18. Bwana, tafadhali tunaomba ulinzi wako juu ya wamisionari wanaofanya kazi katika maeneo magumu.
19. Tafadhali inua wainjilisti wa vitabu, wanafunzi wa kujitolea, waandishi, waliobobea katika masuala ya vyombo vya habari, na wategemezaji kifedha ili kusambaza maneno ya tumaini na uzima.
20. Tunaomba kwa ajili ya shule za Kiadventista, wanafunzi, na waalimu ulimwenguni. Hebu shule hizi zifundishe daima kweli za Biblia na kuwaongoza vijana katika utume na huduma.
21. Bwana, tupatie hekima ya kufikia tamaduni zisizo na dini ambazo hazina shauku katika dini. Mruhusu Roho wako Mtakatifu avunje kuta zinazoizunguka miyo isiyokuwa na dini.
22. Tubariki kadiri tunavyowafikia watu waliofungwa kwa ibada za roho, ibada za sanamu, na imani juu ya wanyama. Tusaidie kuelewa mtazamo wao kwa ulimwengu na kuwatambulisha kwa Mwokozi.
23. Bwana, tafadhali tia msukumo kwa Waadventista wa Sabato ulimwenguni wa kuomba kuliko ilivyowahi kutokea hapo kabla. Tusiadie kusihi pamoja kwa ajili ya mvua ya masika ya Roho Mtakatifu. Tunaomba ukamilisho ulioahidiwa wa Yoeli 2, Hosea 6, na Matendo 2.
24. Tunaomba kwa ajili ya makundi 541 ya watu katika nchi 18 za Divisheni ya Kusini mwa Afrika-Bahari ya Hindi. Tafadhali wangoze katika kweli ya Kibiblia.
25. Tuonyeshe namna ya kufikia mahitaji ya kimwili na kiroho ya wakimbizi. Hebu kanisa letu na lifahamike kwa upendo wetu kwa watu wote, bila kujali walivyo au wanapotoka.
26. Tunaomba kwa uaminifu na ukamilifu ili tutangaze Ujumbe wa Malaika Watatu wa Ufunuo 14. Tuweze kujenga mafundisho yetu yote katika upendo na haki ya Kristo.

27. Tunaomba uinue wamisionari wa mijini ili kupanda makanisa kwa ajili ya makundi 806 ya watu katika nchi 20 za Divisheni ya Inter-Europe.
28. Tafadhali inua jeshi la watenda kazi ili kusimamisha makanisa kwa ajili ya makundi 948 ya watu katika nchi 38 za Divisheni ya Inter-America
29. Tafadhali tufundishe jinsi ya kutangaza Imani zetu za msingi kwa usawa, ubunifu, na uthibitisho wa ki-Biblia. Upendo wa Kristo na uwe kiini cha kila kitu tunachokiamini.
30. Bwana, tafadhali andaa vijana wa kuanzisha makanisa kwa ajili ya makundi 789 ya watu katika nchi 9 za Divisheni ya Kaskazini mwa Amerika.
31. Tunakuomba uandae watakaojitolea kuhudumu katika makundi 70 ya watu katika Fildi ya Israeli.
32. Tunakuomba uinue wamisionari wa kitabibu ili kuanzisha makanisa kati ya makundi 830 ya watu katika nchi 11 za Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati.
33. Tunakuomba uinue mashujaa wa maombi ili waombe maombi ya kuingilia kati kwa ajili ya makundi 2,568 ya watu katika nchi 4 za Divisheni ya Kusini mwa Asia.
34. Tafadhali ruhusu familia zetu kudhihirisha upendo wako katika nyumba zetu na jamii zetu. Tunakuomba ulete uelewano katika familia, ponya mahusiano yaliyovunjika, linda wenyewe hatari ya kukumbwa na unyanyasaji, na dhihirisha nguvu yako ya utakaso katika hali zinazoonekana kutokuwa na tumaini.
35. Tunaomba washiriki wa kanisa letu, wachungaji, na viongozi duniani wajilishe kwa Neno la Mungu kila siku. Tuweze pia kukutafuta kila siku katika maombi binafsi. Tukumbushe kwamba bila wewe, hatuwezi kufanya lo lote.
36. Tunakuomba uinue wauguzi na madaktari ili kuanzisha makanisa kati ya makundi 1,978 ya watu katika nchi 22 za Divisheni ya Afrika Magharibi na Kati.
37. Tunaomba kwa ajili ya watu milioni 49 katika miji 19 ambayo hajafikiwa Zaidi ya Divisheni ya Tran-Europe
38. Tunaomba kwa ajili ya watoto wetu. Tafadhali watie nguvu ili wasimame imara kwa ajili yako wanapokutana na vikwazo na misukumo. Wasaidie kufanya chaguzi sahihi na kusimamia ukweli.
39. Tufundishe kufuata mfano wa Kristo wa kutojifikiria kwa kufikia mahitaji ya kila siku ya watu walio karibu nasi. Tuandae kutumika kama wamisionari wa kitabibu, wanaojitolea kwa ajili ya jamii, na marafiki wa wahitaji.
40. Bwana, tunaomba uamsho mkuu wa utakatifu usafishe kanisa lako katika siku za mwisho. Tunaomba tusimamie ukweli hata mbingu zikianguka.
41. Tunaombea viongozi wa vijana ulimwenguni walio waaminifu katika kuhamisha hazina yetu katika kizazi kinachofuata: *utambulisho* katika Kristo, *utume* kama Waadventista wa Sabato, na *uongozi* katika kanisa mahalia.

42. Tunaombea vijana wanaoishi katika hatari kwa ajili ya Bwana kupitia Harakati ya OYiM (One Year in Mission) na harakati ya Mission Caleb.
43. Bwana, tafadhali tuonyeshe mkakati uliokubaliwa na Mungu wa kufikia Yeriko ya dunia kwa Ujumbe wa Malaika Watatu na kuongoza akina Rahabu katika kila mji kwenye wokovu katika Kristo.
44. Bwana, tafadhali leta uponyaji na amani kwa mamilioni ya wanaoteseka kwa magonjwa. Tuonyeshe namna tunavyoweza kuwa mikono na miguu yako ili kuwabariki wanaoteseka na kuleta tumaini kwa wenye hofu.

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamshowww.tendaysofprayer.org*Siku ya Kwanza***Zawadi ya Yesu ya Pekee zaidi**

Fungu Elekezi: “Je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao!” Matendo 1:8

Sina Kitu

Wanafunzi wake waliomba kuwa, “Bwana, tufundishe Kuomba!” Walikuwa wameona namna Yesu alivyouniganika daima na Baba yake wa Mbinguni na kutamani nguvu iyo hiyo katika maisha yao wenywewe.

Yesu aliitikia kwa somo la maombi la kukumbukwa lililogawanyika katika sehemu tatu: sehemu ya kwanza ni Sala ya Bwana, sehemu ya pili ni mfano wa rafiki aliyejeka usiku wa manane, na sehemu ya tatu – katika kilele chake – ni hitaji la kuomba Roho Mtakatifu bila kukoma (Luka 11:1-13).

Katika mfano huo (fungu la 5-8), kuna mtu asiyé na kitu cha kumlisha mgeni wake aliyefika kwa kuchelewa. Mtu huyo anaharakisha kwenda kwa jirani yake na kuomba amkopeshe mikate mitatu ili kumlisha mgeni wake, akieleza, “Sina kitu.” Anaendelea kuomba hadi hatimaye anapewa mikate ili kushiriki na mgeni wake. Katika kisa hiki tunaona kwamba tunapaswa kuja kwa Yesu ili kuwa na kitu cha kushiriki na wengine. Tunapotaka kutoa Mkate wa Uzima, mara nyingi tunatambua kwamba hatuna cho chote cha kutoa!

Kisha Yesu anaunganisha tatizo katika mfano huu (*Sina kitu*) pamoja na hitaji letu la kumuomba Roho Mtakatifu: “Nami nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa” (Luka 11:9).

Yesu Anatualika: Dumu Kuomba

Hapa katika Luka 11, Yesu anasisitiza mara 10 kwamba tunapaswa kumuomba Roho Mtakatifu katika maisha yetu. Sifahamu fungu jingine anapotusihii kwa upendo mwingu kuzingatia moyoni kitu fulani.

“Nami nawaambia, **Ombeni**, nanyi mtapewa; **tafuteni**, nanyi mtaona; **bisheni**, nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila **aombaye** hupokea; naye **atafutaye** huona; naye **abishaye** atafunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawawe **akimwomba** mkate,

atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au **akimwomba** yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao **wamwombao!**" (Luka 11:9-13).

Katika mafungu haya machache, Yesu anatumia kitenzi *omba* mara sita na anaweka mkazo katika dhana ya *kutafuta* mara mbili na *kubisha* mara mbili. Hivi vyote ni vitenzi vyta kitendo. Anaonyesha dhahiri kwamba tunapaswa kutenda ili kujazwa na Roho Mtakatifu. Matumizi ya mwisho ya *omba* yapo katika wakati endelevu kwa Kiyunani, ikimaanisha kwamba tunapaswa kuomba wala siyo mara moja tu bali kudumu kuomba – kwa uendelevu. Kwa uwazi, Yesu anataka kuamsha tamanio letu la Roho Mtakatifu kwa mwaliko huu wa moyoni. Anafahamu kwamba tunakosa kitu cha muhimu tusipoomba mibaraka mingi ya Roho Mtakatifu kwa namna endelevu.

Katika kitabu cha *Christ's Object Lessons* tunasoma kuwa, "Mungu hasemi, omba mara moja, na utapokea. Anatusihi tuombe. Tudumu katika maombi bila kusita. Dumu bila kuchoka katika maombi. Kuomba kwa kudumu humweka mwombaji katika hali ya bidii zaidi, na humpatia shauku iliyongezeka ya kupokea vitu anavyoviomba" (uk. 145).

Hebu fikiria kwa muda, kwa nini Yesu mwenyewe alitumia muda mwingi sana katika maombi ya kila siku? Ellen White anaeleza kuwa, "Asubuhi kwa asubuhi aliwasiliana na Baba yake aliye mbinguni, akipokea kutoka kwake kila siku ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu" (*Signs of the Times*, Nov. 21, 1985).

Kwa hakika, Yesu alikuwa mfano wetu katika hili. Jiulize kuwa: Ikiwa Yesu alihitaji matengenezo mapya kila siku kutoka kwa Roho Mtakatifu, ni muhimu zaidi kiasi gani kwangu?

Ushuhuda na Changamoto kutoka kwa Mshiriki wa Kanisa

"Kwa miaka miwili iliyopita nimekuwa nikiomba kila siku kwa ajili ya umwagawaji wa Roho Mtakatifu katika maisha yangu... Safari yangu na Mungu imekua ya kushangaza. Tunda la Roho katika Wagalatia 5 limekuwa dhahiri zaidi katika maisha yangu tangu nilipomwomba Yesu akae ndani yangu, afanye mapenzi yake ndani yangu, na kunifanya upya kila siku kupitia kwa Roho Mtakatifu. Nina furaha kubwa zaidi katika kusoma Biblia na kumshiriki Kristo na wengine, na nina shauku kuu ya kuombea wengine; zaidi ya hayo, mtindo wangu wa maisha umebadilika sana... Ninakupatia changamoto ya kuomba kila siku kwa majuma sita ili kujazwa Roho Mtakatifu upate kuona kile kinachotokea" (C.H.).

Kuomba Neno la Mungu

Kwa nini hatupati majibu zaidi kwa maombi?

"Wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi! Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu" (Yakobo 4:2, 3).

Mpendwa Baba wa Mbinguni, tafadhali tusamehe kwa kupuuzia kudumu kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Asante kwamba tukiungama dhambi zetu, wewe ni mwaminifu na wa haki utatusamehe.

Mahitaji yetu huonyesha jinsi tunavyothamini kile Mungu anachotoa.

"Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao!" (Luka 11:13).

Mpendwa Bwana, asante kwa kutoa mito ya maji ya uzima kwa wale wanaokuamini. Tafadhali tusaidie kuishi tukijisalimisha kila siku tukidumu hivyo kwa Kristo ili uweze kuitimiza ahadi hii katika maisha yetu.

Mapendelekezo zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.

Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Mapendelekezo ya Nyimbo

Saa Heri ya Maombi (#135)

Nijaze Sasa (#40)

Zitakuwa Nyota Tajini (#58)

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamshowww.tendaysofprayer.org*Siku ya Pili***Kushikilia Zawadi**

Fungu Elekezi: “ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo” Waefeso 3:18-19.

Pokea, Salimisha, Kua

Ni kwa namna gani tunaweza kupata uzoefu wa upendo wa Mungu kwa ukamilifu? Soma kile anachosema mtume Paulo katika Waefeso 3:14-21.

1. Kwanza, unahitaji kupokea karama ya Roho Mtaktifu. “Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani” (fungu la 16).
2. Kisha, tunasalimisha maisha yetu kwa Kristo na kuishi katika uhusiano wa karibu, na endelevu pamoja naye “Kristo akae miyoni mwenu kwa imani” (fungu la 17).
3. Kisha imani yetu hukua na kukomaa kuitia kwa Kristo na Roho Mtakatifu ndani yetu. Tunakuwa “na shina na msingi katika upendo” (fungu la 17).

Matokeo ni nini? Tunapata uzoefu wa upendo wa Mungu kwa ukamilifu. Anatupatia nguvu “ili tupate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo” (fungu la 18).

Upendo wa Kristo Hupita Kila Jaribu

Fikiria mfano wa Mwana Mpotevu katika Luka 15:11-32. Siku moja kijana mdogo alimwendea baba yake (aliywakilisha Mungu) na kutangaza kwamba alitaka kuondoka nyumbani na kuishi maisha yake mwenyewe. Ni dhahiri aliona kwamba sheria za nyumba ya baba yake (amri za Mungu) hazikumpendeza. Kijana akadai urithi wake, ambao hata hakuwa amepangiwa kwa wakati ule, hivyo baba alimpatica sehemu yake. Baba akampatia uhuru kamili kwa sababu alimpenda na aliheshimu maamuzi yake (kama Mungu anavyotutendea).

Kisha kijana akasafiri kwenda nchi ya mbali na kuendelea kutumia fedha zake kwa sherehe za anasa na wanawake. Kadiri fedha ilivyoisha, ndivyo mduara wake wa “marafiki” ulivyozidi kupungua, hatimaye alibaki bila kitu cho chote. Ubaya zaidi, njaa

ikaipiga nchi ile aliyokuwa akiishi. Akiwa na shauku kuu ya kuishi, alitafuta kazi, lakini sehemu pekee aliyopata ni kazi ya kulisha nguruwe. Njaa ikamtesa, akawa akitamani kujishibisha kwa maganda waliyokula nguruwe, wala hapana mtu aliyempa kitu

Kama itokeavyo mara nyingi hali inapokuwa ngumu kumzidi mtu, alianzai kufikiria maisha yake. Aligundua kwamba watenda kazi wote wa baba yake walikuwa na chakula cha kutosha wakati yeye alikua akishinda njaa, hivyo aliamua kurudi kwa baba yake na kusema, "Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako" (fungu la 18, 19)

Kijana akaanza safari ya kwenda nyumbani akiwa na hisia mkanganyiko, lakini tayari baba alikuwa akimsubiri. Huyu Baba akiwa amejawa na huruma, alimkimbila na kumkumbatia kijana wake, akambusu, licha ya kijana kuwa mchafu na mwenye kunuka. Kabla ya kijana kumaliza ungamo lake lote, baba aliagiza watumishi wake kuleta nguo nzuri na kuandaa sherehe. Ni wazi kwamba alimpenda kijana wake kama ilivyo kuwa hapo kabla. Katika kisa hiki tunapata kisa kizima cha wokovu – kutubu na kuungama kwa wenye dhambi, Baba anayesubiri kwa upendo, na ukaribisho wa furaha tunaporudi. Mungu anatupenda sana! Lakini tunahitaji kumwendea, kama kijana alivyorudi kwa baba yake. Upendo wa Mungu hupita kila jaribu! Hatashindwa kukukaribisha.

Ni pale tu kijana aliporudi ndipo baba alipoweza kumwaga upendo wake wote. Ni hapo tu ndipo kijana alipokuwa huru kupokea vyote ambavyo baba alitaka kumpatia. Hatimaye hakuna kilichoziua uhusiano wao wa karibu, na kijana aliweza kupata uzoefu wa wema kamili wa baba yake, ambaye kamwe hakuacha kumsubiri.

Tukirudi katika swalı – tunawezaje kupata uzoefu kamili wa upendo wa Mungu? Kwa kuishi kwa ukamilifu, tukijisalimisha kila siku kwa Kristo kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Na upendo wa Mungu unapojaza maisha yetu, tunakuwa mifereji ya upendo wake kwa wengine; kadiri tunavyotoa zaidi, ndivyo tunavyopokea zaidi. Ellen White anasema, "Unahitaji ubatizo wa kila siku wa upendo ambao katika siku za mitume uliwafanya kuwa wamoja" (*Testimonies for the Church*, gombo la 8, uk. 191).

Na kwa nini ni muhimu sana kuuelewa upendo huu wa kimbingu? "Paulo aliona kwamba tabia ya Kristo inapaswa kueleweka kabla watu hawajampenda au kuutazama msalama kwa jicho la tumaini. Hapa kunapaswa kuanza kule kujifunza ambako kutakuwa ndiyo sayansi na wimbo wa waliokombelwa milele zote" (*The Acts of the Apostles*, uk. 273). Ni furaha iliyoje kujifunza upendo wa Mwokozi wetu usiofananishwa, wenye sura nyingi! Je, hautachagua leo kugeuza macho yako kumtazama Yesu?

Kuomba Neno la Mungu

Ni amri ipi iliyo Kuu?

“Akamwambia, ‘Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote’... Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, ‘Mpende jirani yako kama nafsi yako’” (Mathayo 22:37, 39).

Baba, asante kwa kunipenda. Tafadhali nisaidie kukupenda kwa moyo wangu wote, kwa mwili wangu wote, kwa hisia zangu zote, kwa nguvu zangu zote. Asante kwa kujibu ombi hili kulingana na mapenzi yako. Ninataka kumpenda jirani yangu kwa msaada wako. Nifanye kuwa mfereji wa upendo wako.

Ni kwa namna gani tunaweza kufahamu kina cha upendo wa Mungu?

“Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. Kristo akae miyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo” (Waefeso 3:16-19)

Baba, ninaomba uniiamarishe ndani na nje kupitia kwa Roho wako Mtakatifu. Hebu Kristo aishi ndani yangu kwa imani na kuniongoza ili njengwe imara katika upendo wake. Kwa sababu ombi hili ni kulingana na mapenzi yako, ninakushukuru kwa kunisikia na kunijibu.

Mapendeleko zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.

Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Mapendeleko ya Nyimbo

Yesu kwa imani (#123)

Mungu atukuzwe (#3)

Ninakupenda Zaidi (#48)

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamshowww.tendaysofprayer.org*Siku ya Tatu***Ufunguo ni Kujisalimisha**

Fungu Elekezi: “*Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndi ibada yenu yenze maana*” Warumi 12:1.

Safari Yangu

Nilikuwa mfanya biashara, mwenye umri wa miaka 36 pale rafiki yangu aliyekuwa mchungaji alipofariki ghafla katika umri wa miaka 41. Jambo hili lilileta swali akilini mwangu: ni jambo gani lingetokea kama Mungu angeniita kuwa mchungaji? Sikutaka kabisa kuwa mchungaji. Kwa muda wa wiki nzima nilipambana sana na kushauriana na Mungu - asubuhi, mchanana, na jioni. Nilimwelezea namna ambavyo ningeweza kumtumikia kwa njia zingine. Lakini hakuwa akisikiliza kukataa kwangu, na kadiri nilivyopiga magoti kitandani kwangu bila hoja za ziada, wazo la kimya liliingia akilini mwangu: *Mungu anakupenda!* Na niliwaza, *Ni kweli, naamini ananipenda.*

Baada ya dakika chache, Imani kwa upendo wa Mungu iliniongoza kujitoa kikamilifu. Ndipo nilipopata amani. Na mwaka mmoja na nusu baadaye, Bwana aliniita kuwa mchungaji. Miaka mingi imeshapita baada ya hapo, lakini bado ninamshukuru. Ulikuwa ni upendo wake usio na kikomo na hekima yake iliyonionyesha njia tofauti kabisa na ile niliyokuwa nayo akilini. Sasa ninaona kwamba kujitoa huku kuliachia mibaraka mikubwa katika maisha yangu. Mungu aliniongoza katika njia bora Zaidi.

Kwa nini Kujisalimisha?

Kama anavyoandika Garrie F. Williams kuwa, “Kujisalimisha kikamilifu ndio ufunguo wa wokovu, wa kuzaliwa upya, na wa ushindi dhidi ya dhambi na majaribu, na kwa ukamilifu wa Roho Mtakatifu” (*How to be Filled with the Holy Spirit and Know It – Namna ya kujazwa na Roho Mtakatifu na Kufahamu hivyo*). Ni vigumu kukazia ujumbe huu wa kutia moyo Zaidi ya hapo.

Kama ilivyonipasa kujisalimisha kabla Mungu hajanitumia kimamilifu, ndivyo mtume Paulo alivyopaswa kuacha maisha na mipango yake ya kale pale Mungu alipomuita njiani alipokuwa akielekea Dameski. Katika barua yake kwa Warumi, baadaye Paulo

anawasihi waamini kuwa "itoeni miili yenu iwe dhabihu hai" na "viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki" (Warumi 12:1; 6:13).

Wengi hawajajisalimisha kwa Mungu (mara nyingi kwa kupuuzia) lakini badala yake wameshikilia maisha yao mikononi mwao wenyewe. Wanapungukiwa nguvu ya Roho Mtakatifu, ambayo ni karama inayoleta karama zingine zote za Mungu. "Lakini kama ahadi nyingine yo yote, hutolewa kwa masharti. Kuna wengi wanaoamini na kuchukua hatua kutangaza ahadi ya Mungu; *wanazungumza kumhusu* Roho Mtakatifu, lakini hawapati faida yo yote. Hawasalimishi nafsi ili iongozwe na mamlaka za kimbunguni" (*The Desire of Ages*, uk. 672).

Kama wanadamu tunapinga kusalimisha uhuru wetu, lakini shauku ya Mungu kwetu ni kinyume: "Mungu anatamani kutuponya, kutuweka huru. Lakini kwa sababu hili huhitaji kubadilika kikamilifu, kufanywa upya kwa asili yetu yote, tunapaswa kujitegemeza kikamilifu kwake" (*Steps to Christ*, uk.43).

Maisha ya dhambi si maisha huru kama wengi wetu tunavyodhani. "Kila nafsi inavyokataa kujitoa kwa Mungu ipo chini ya nguvu nyingine. Si yeye. Anaweza kuongea kwa uhuru, lakini yupo katika utumwa wa hali ya juu. Haruhusiwi kuuona uzuri wa kweli, kwa kuwa akili yake ipo chini ya uongozi wa Shetani. Wakati akijisifu kwamba anafuata uongozi wa maamuzi yake, ni kinyume chake, anakuwa anatii nia ya mfalme wa giza. Kristo alikuja kuvunja vifungo vya utumwa wa dhambi kutoka kwa kila nafsi" (*The Desire of Ages*, uk.466).

Tunapoteza nini kwa kujisalimisha kwa Kristo? Ana uwezo wa kutuweka huru kutoka katika udhalimu wetu wenyewe – kutoka katika wivu, katika chuki, katika ugomvi, katika tamaa, katika uraibu, katika kiburi, katika kukata tamaa, katika hali duni, na Zaidi. Kumbuka kuwa, kila mwanadamu ni tatizo lake mwenyewe. *Wewe ni tatizo kubwa Zaidi kwako mwenyewe.* "Katika badiliko linalotokea pale nafsi inapojisalimisha kwa Kristo, kuna hisia ya hali ya juu Zaidi ya uhuru" (*The Desire of Ages*, uk.466).

Lakini mfinyanzi anaweza kutenda kazi tu kwa kutumia udongo ulio mikononi mwake. Ndiyo maana tunajitoa kwa Mungu. "Kusalimisha nguvu zetu zote kwa Mungu hurahisisha tatizo la maisha. Huhafisha na kupunguza maelfu ya mapambano dhidi ya tamaa za moyo wa asili" (*My Life Today*, uk.6).

Kujisalimisha pekee huleta furaha idumuyo. "Wale wanaoamini neno la Kristo, na kusalimisha nafsi zao kwa ulinzi wake, maisha yao kwa uongozi wake, watapata Amani na utulivu. Hakuna cho chote cha ulimwengu huu kinachoweza kuwafanya wawe na

huzuni Yesu anapowafanya wafurahi kwa uwepo wake. Katika ukubali mkamilifu kuna pumziko kamilifu” (*The Desire of Ages*, uk. 331). Anakualika leo kupata uzoefu wa pumziko hilo kamilifu!

Kuomba Neno la Mungu

Tufanye vyombo ya upendo wako.

“Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viugo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki” (Warumi 6:13).

Bwana, tunataka kukupatia kila sehemu ya maisha yetu. Tutumie kama vyombo kwa utukufu wako.

Fanya maisha yetu yawe ibada

“Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenze maana” (Warumi 12:1).

Baba, ahsante sana kwa kutualika kuwa viumbe vipyta. Tuonyeshe namna ya kujisalimisha kila siku kwako bila vizuizi vyo vyote. Tusaidie kukufuata katika mambo yote kwa nguvu zako.

Tulinde na Muovu.

“Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali ye ye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mweovu hamgusi” (1 Yohana 5:18).

Bwana, ahsante kwa kuahidi kutulinda dhidi ya muovu pale tunapojisalimisha kwako. Tuongoze katika njia yako kuielekea furaha kamili.

Mapendelezo zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.

Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Mapendelezo ya Nyimbo

Yote kwa Yesu (#122)

Hivi Nilivyo Unitwae (#140)

Ni Salama Rohoni Mwangu (#127)

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamshowww.tendaysofprayer.org

Siku ya Nne

Kuweka Uamsho Katika Utendaji

Fungu Elekezi: “*Wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi. Haa mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu*” Yakobo 4:2, 3.

Vuta Taswira ya Yale Yanayowezekana

Fikiria kwamba mtu anatoa somo la uamsho kanisani kwako. Akitoa wito, mhubiri anawaalika wasikilizaji kumkubali Yesu na kumfuata daima. Pengine hakuna anayeitikia. Pengine watakaoitikia ni wachache, au pengine ni wengi. Kwa sababu Mungu aliumba viumbe walio na uhuru wa kuchagua, hatuwezi kuamua namna wengine watakavyoitikia mwaliko huo. Lakini, bado wengi wanapokubali ujumbe wa Mungu na kuufanya kazi – ikiwa ujumbe huo umetokana na mahubiri ya hadhara, masomo binafsi ya Biblia, uinjilisi wa marafiki, au matukio ya kushangaza ya kimbingu – ni wazi kwamba ushuhuda wetu umekuwa wenyewe mafanikio. Aina hii ya mafanikio ni karama ya Roho Mtakatifu. Tunasimama – tukishangaa- na kumtazama Mungu akitenda miujiza.

Lakini mara nyingi maisha ya Wakristo huwa na mafanikio hafifu. Hii haimaanishi kwamba programu za kanisa letu na mipango ya kuwafikia wengine ni dhaifu au ni ya bure. Bwana amebariki – kwa kadiri iwezekanavyo – jitihada zetu za kibinadamu za dhati. Lakini uzoefu wetu ungekuwa mkubwa kiasi gani kama tungepokea kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa ujazo wote? Ni Mungu pekee anayejua yale yanayoweza kutokea! Mhubiri Henry T. Blackaby anaandika, “Atakamilisha mengi zaidi ndani ya miezi sita kupitia watu waliojitoa kwake, kuliko tunavyoweza kukamilisha kwa nguvu na hekima yetu wenyewe kwa miaka sita.” (Blackaby, *Experiencing God*, uk. 108).

Ni muhimu kuomba kwa ajili ya uamsho, lakini hatuwezi kuachia hapo. Ninakualika kuchukua hatua muhimu za *kupata uzoefu* halisi wa uamsho binafsi. Kwa mibaraka ya Mungu, maisha yako yanaweza kuwa na nguvu Zaidi na makamilifu kuliko ilivyowahi kuwa hapo kabla. Nyumba yako na kanisa lako pia linaweza kupata uzoefu wa maisha mapya.

Ni nini Kinakosekana?

Kwanza kabisa, kuna maswali hapa: Ni nini kiini cha matatizo yetu yote? Je, ni masuala ya kiroho? Je, upungufu wetu wa Roho Mtakatifu unaweza kuwa ndicho kiini cha uzoefu wetu wa Kikristo ulio wa uvuguvugu? Ikiwa jibu ni ndiyo, ni *kwa nini* basi tuna ukosefu wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu?

Jibu la Biblia: "... Wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi. Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu" (Yakobo 4:2, 3). Kama tulivyojifunza katika somo la Siku ya 1, Mungu anatuita *tumwombe* Roho Mtakatifu daima katika maisha yetu. "Kwa nini hatuwi na njaa na kiu ya karama ya Roho, kwa sababu hii ndiyo njia tunayoweza kupokea nguvu? Kwa nini hatuizungumzii, hatuiombi, hatuhubiri kuhusu karama hii?" (*Testimonies for the Church*, gombo la 8, uk.22).

Yakobo pia anaeleza kwamba, "Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu.." Pengine anamaanisha kwamba Mungu hawezi kubariki ikiwa akili zetu zimeelekezwa katika "mambo ya mwili." Paulo anaelezea kuwa, "Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na Amani" (Warumi 8:5, 6).

"Nia ya mwili" anayoizungumzia Paulo ni nini? Kwa kweli, Neno la Mungu huelezea makundi matatu ya watu na uhusiano wao pamoja nae. Katika kila kundi kuna tofauti nyingi kutokana na malezi, tabia za kurithi, kujitawala, umri, tamaduni, elimu, na mengine. Lakini licha ya tofauti hizi, tunapata makundi matatu tu makuu: kundi la yule wa "asilia" au mtu wa "ulimwengu," kundi la yule wa "kiroho" au mtu "aliyejazwa roho," na kundi la yule "mwenye nia ya mwili" au mtu "wa mwili."

Makundi haya matatu yanaelezewa katika 1 Wakorintho 2:14-16 and 3:1-4. Kwa sasa tutataja tu mtu wa asili katika kupita; anaishi ulimwenguni lakini bado hana uhusiano na mungu. Washiriki wa kanisa hupatikana katika makundi mengine mawili, na mtazamo wa haraka kwa kila maelezo kutasaidia kudhihirisa mahali tatizo lilipofichwa. Swali ni kwamba ni hili, nipo kundi gani? Uchunguzi mfupi unapaswa kusaidia kujitathmini - tukiweka akilini kwamba tunataka kutazama maisha yetu wenyewe, na si maisha ya wengine! Wewe ni mtu wa aina gani?

Wa Asili: Hana uhusiano na Mungu. "Hayapokei mambo ya Roho wa Mungu, maana kwake huyo ni upuuzi" (1 Wakorintho 2:14).

Wa Kiroho: Ana uhusiano mkamilifu, na halisi na Mungu. Tunapokuwa wa kiroho, "tunakuwa na nia[Roho] ya Kristo" (1 Wakorintho 2:16).

Wa Mwili: Ana uhusiano wenyе hofu au uliogawanywa pamoja na Mungu. "Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenyе tabia ya rohoni, bali kama na watu wenyе tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo" (1 Wakorintho 3:1).

Tukifika Siku ya 5: Ni nini tofauti kati ya Mkristo wa kiroho na wa kimwili?

Kuomba Neno la Mungu

Roho Mtakatifu huongoza mawazo yetu.

"Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waufuatao roho huyafikiri mambo ya roho" (Warumi 8:5).

Baba, tunafahamu kwamba pengine tupo chini ya mvuto wa miili yetu au wa Roho Mtakatifu. Tafadhali tufanye tuwe Wakristo wa kiroho na elekeza mawazo yetu kwa mambo ya Roho.

Hatupo tena chini ya huruma za tamaa zetu.

"Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili" (Wagalatia 5:16).

Bwana, ahsante kwa sababu Roho Mtakatifu huvunja nguvu za dhambi katika maisha yetu. Tafadhali kuza tunda la Roho katika mioyo yetu. Tunakushukuru kwa ahadi hii ya pekee.

Roho hutuokoa kutoka katika hukumu.

"Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti" (Warumi 8:1, 2).

Baba, ni mbaraka ulioje kufahamu kwamba kifungo cha dhambi kimevunjwa tunapoishi ndani ya Roho Mtakatifu. Asante yaa ajili ta Kristo aliyebeba hatia yetu juu yake mwenyewe na kutuweka huru kutoka katika dhambina mauti.

Mapendelezo zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.
Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.
Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Mapendelezo ya Nyimbo

Furaha Gani (#43)

Moyo Safi (#116)

Umechoka Umesumbuka (#124)

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamsho

www.tendaysofprayer.org

Siku ya Tano

Kuwa Wa Kiroho au wa Kimwili: Tofauti ni Nini?

Fungu Elekezi: “Lakini sisi tunayo nia ya Kristo” 1 Wakorintho 2:16.

Kiunganishi Chetu Mbinguni

Kabla ya kuelezea Wakristo wa kiroho na wa kimwili, tunapaswa kukumbuka kwamba hatuzungumzi kuhusu “wenye dhambi” na “wasio na dhambi.” Watu wote, wa kiroho na wa kimwili, ni wadhambi wanaohitaji Mwokozi. Haki yetu pekee huja kutoka kwake. Badala yake, kigezo cha kuwa katika kundi moja au lingine ni uhusiao wetu binafsi na Roho Mtakatifu. Mungu ameainisha kwamba hatuweza kugawanya uhusiano wetu na Roho Mtakatifu bila kuharibu muunganiko wetu na mbingu (Mathayo 12:32). Ellen White anaeleza kuwa, “yule anayeikataa kazi ya Roho Mtakatifu anajiweka sehemu ambapo kuungama na Imani haviwezi kumfikia. Ni kwa Roho wa Mungu atendaye kazi ndani ya moyo” (*The Desire of Ages*, uk.322).

Na inastahili kurudiwa: mtu pekee ninayepaswa kumtathmini kama wa kiroho au wa kimwili ni mimi mwenyewe. Mungu anaweza kutenda kazi katika mioyo mingine na hahitaji niwanyoshee vidole washiriki wenzangu. Habari njema ni kwamba ikiwa sijafurahishwa na kile anachodhihirisha katika moyo wangu, anaweza kunibadilisha tangu leo!

Mshiriki wa Kiroho

Mtu wa kiroho ni Mkristo aliyebadilishwa kweli kweli. Ingawa amezaliwa mwenye dhambi, anaitwa “wa kiroho” kwa sababu ana uhusiano ulio hai na unaokua pamoja na Roho Mtakatifu. Mtume Paulo anaandika, “Lakini mtu wa rohoni huyatambua yote, wala ye ye hatambuliwi na mtu. Maana, ‘ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimeshe?’ Lakini sisi tunayo nia [Roho] ya Kristo” (1 Wakorintho 2:15, 16).

Yesu ndiye kiini cha maisha ya mtu wa kiroho na hutawala ndani ya moyo wake na kutambua vipaumbele vyake. Mtu wa kiroho amejitoa kikamilifu kwa Yesu naye anaomba daima kwa ajili ya Roho Mtakatifu (Luka 11:13). Katika muktadha wa Laodikia,

mtu wa kiroho anaweza kuitwa "moto" (Ufunuo 3:15). Katika mfano wa wanawali 10, anaweza kuitwa "mwenye hekima" (Mathayo 25:2-4). Mtu wa kiroho hupata uzoefu wa uzima "tele" (Yohana 10:10) na hujazwa na "utimilifu wote wa Mungu" (Waefeso 3:19). Anafurahi kwamba "ameokolewa kwa imani" (Waefeso 2:8). Japo mtu huyu wa kiroho hupitia vikwazo na majaribu, daima huelekeza macho yake kumtazama Yesu.

Mshiriki wa Kimwili

Mtu wa kimwili anaweza kuwa na uhusiano wa kujifanya au uliogawanyika kwa Mungu. Anaweza kuwa tofauti na Roho Mtakatifu komyakimya au hata mwenye uasi wa waziwazi. Hili ndilo asemalo mtume Paulo: "Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenyetabia ya rohoni, bali kama na watu wenyetabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi, kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu? Maana hapo mtu mmoja asemapo, Mimi ni wa Paulo; na mwingine, Mimi ni wa Apolo, je! Ninyi si wanadamu? (1 Wakorintho 3:1-4).

Hapa tunahitimisha kwamba sifa bainishi inapaswa kuwa ni uhusiano wetu na Roho Mtakatifu. *Wa Mwili* humwelezea mtu anayeishi kwa mwili; kwamba ni kwa nguvu za kawaida za kibinadamu, si kwa Roho Mtakatifu. Na janga kubwa Zaidi ni kuwa hajachagua kupokea uzima wa milele (Warumi 8:9).

Paulo anawaelezea watu wa mwili kama "ndugu," ambayo huonyesha kwamba walikuwa washiriki wa kanisa. Hakuweza kuwaita "wa kiroho" kwa sababu hawakujazwa kwa ukamilifu na Roho Mtakatifu. Hawakukua katika Imani kama walivyopaswa. Inawezekana ukawa mshiriki wa kanisa kwa miaka mingi na bado ukawa Mkristo wa kimwili. Inawezekana ukawa na ufahamu wa Kibiblia na bado usiwe mkomavu kiroho. Wakristo wengi wa kimwili huhisi kutoridhika, kutofurahi, au kukosa kusudi katika maisha yao ya kiroho. Baadhi ni watu wasio na huruma na husema, "Sisi ni wenyetabia. Hatuwezi kufanya lo lote juu ya hilo."

Wakristo wengine wa kimwili ni wenyetabia shauku na walio hai, pengine hujivunia nafasi zao za muhimu kanisani. Jambo la kusikitisha, Yesu anasema kuwa, "Wengi wataniambia siku ile, 'Bwana, Bwana, hatukufaya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?' Ndipo nitawaambia Dhahiri, 'Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu!'" (Mathayo 7:22, 23).

Tatizo ni nini? Hawakuwa na uhusiano binafsi na Yesu na muunganiko ulio hai na Roho Mtakatifu.

Ukitambua kuwa wewe ni Mkristo wa kimwili kwa sasa, usife moyo! Una uwezekano wa maisha mapya kwanzia sasa. Wakristo wengi wa kimwili wapo katika hali hii bila kufahamu, na tayari unawenza kuwa unaomba kwa ajili ya uzoefu wa Imani wa kina ziasi. Yesu anatamani “furaha yako itimizwe” (Yohana 15:11), na anakualika kumpumzika katika tumaini kuu la uzima wa milele.

Kuomba Neno la Mungu

Bado tu wa kimwili, lakini kuna tumaini.

“Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama watu wenye tabia za rohoni, bali kama wati wemue tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Niliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi. Kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?” (1 Wakorintho 3:1-3).

Mpendwa Bwana, ahsante kwa kujumuisha maneno “hata sasa” katika mafungu haya, kwa sababu hutukumbusha kwamba hatuhitaji kubaki katika hali hii. Tunataka utubadilishe leo. Ahsante kwamba husuda, fitina, na migawanyiko huponywa tunapoishi ndani ya Roho Mtakatifu.

Je, tunaomba tukiwa na nia ya kimwili?

“Wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi. Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu” (Yakobo 4:2, 3).

Baba, tunaishi katika umasikini wa kiroho kwa sababu hatuombi, au tunaomba tukiwa na ubinafsi, nia za kibinadamu. Tafadhali badili maombi yetu na utuongoze kwa Roho Mtakatifu.

Mapendeleko zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.

Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Mapendelezo ya Nyimbo

Kuwa na Yesu (#51)

Nimekombolewa na Yesu (#35)

Wimbi Litakasalao (#188)

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamshowww.tendaysofprayer.org*Siku ya Sita***Ufumbuzi wa Mungu kwa Mahangaiko Yetu**

Fungu Elekezi: “Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha” Luka 9:23, 24.

Siri Mbili za Uamsho Unaodumu

Yesu anatoa suluhisho kwa Wakristo wa kimwili wanaotaka kuwa Wakristo wa kiroho. Anasema, “Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu” (Yohana 15:4). Kwa maneno mengine, “Dumuni ndani yangu.” Lakini ni kwa namna gani?

Ellen White anasema kwamba kukaa ndani ya Kristo humaanisha –

1. “**kupokea Roho wake daima**” na
2. “**maisha ya kujisalimisha kikamilifu** katika utumishi wake” (*The Desire of Ages*, uk.676)

Suluhisho hili la kimbingu lenye sehemu mbili huongoza, siyo tu katika uamsho, bali pia katika maisha ya Kikristo yenye furaha. Kwa nini? Yesu alisema, “Hayo nimewaambia, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe” (Yohana 15:11). Kwa kufuata hatua hizi mbili, tunapata uzoefu wa “Kristo ndani yako,” au uwepo wake katika maisha yetu ya kila siku, na maana yake ni kwamba tunashiriki tumaini la utukufu wake (Wakolosai 1:27).

Kipengele muhimu: Kila siku tunaomba na kupokea kwa imani kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, na kila siku tunasalimisha kila tulicho nacho na jinsi tulivyo kwa Mungu. Yeye hutoa furaha!

Katika somo la Siku ya 1 tulizungumza kuhusu namna ilivyo muhimu kuomba Roho Mtakatifu, na katika somo la Siku ya 3 tulijifunza hitaji letu la kujisalimisha. Leo tutaangalia hatua nyingine mbili – tukiwa na mtazamo maalumu katika hitaji letu la kuomba na kujisalimisha *kila siku*.

Kwa nini Tuombe Kila Siku kwa ajili ya Roho Mtakatifu?

Miaka iliyopita nilisoma kisa cha jambazi mmoja aliyemgeukia Kristo. Kwa moyo wote alikiri uongo wake, wizi, na makosa mengine mengi aliyokuwa amefanya, na matokeo yalikuwa ni uzoefu wa kuingilia kati kwa kimbingu. Mungu aligeuza kabisa maisha yake.

Hili lilinigusa. Nikajambia, "...niko sawa kwa njia nydingi, lakini sina uzoefu kama huo. Hivyo nikaomba kuwa, "Bwana, ninataka pia kuungama dhambi zangu zote zinazofahamika na dhambi ambazo bado hujanionyesha. Zaidi, nitaamka saa moja kabla kila siku ili kuomba na kusoma Biblia. Ninataka kuona kama utaingilia kati pia katika maisha yangu."

Mungu atukuzwe, kwa kuwa aliingilia kati katika miasha yangu! Si kwa sababu nilipata faida kwa kuamka mapema lakini kwa sababu kila siku nilijiweka pale ambapo Roho Mtakatifu angeweza kunipata. Kama ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu ulikuwa ni hitaji la kila siku kwa Yesu katika dunia hii, ni kwa kiasi gani tunahitaji zaidi nguvu hii? Paulo anaandika kumhusu mtu wa rohoni "akifanywa upya siku hata siku," na anaomba kwamba watu wa Mungu "kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani" (1 Wakorintho 4:16, Waefeso 3:16). Na Ellen White anatoa tumaini hili: "Bwana yu tayari zaidi kumtoa Roho mtakatifu kwa wale wanaomtumikia kuliko wazazi wawapavyo zawadi njema watoto wao. Kwa ubatizo wa kila siku wa Roho, kila mtendakazi anapaswa kutoa ombi lake kwa Mungu" (*The Desire of Ages*, uk.50). "Utu wetu wa ndani" unahitaji matunzo ya kila siku.

Kwa nini Tunapaswa Kujisalimisha Kila Siku kwa Yesu?

Akijaribu kuwasaidia wanafunzi wake kuelewa asili ya kujitoa ya uanafunzi, Yesu aliwaambia, "Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate" (Luka 9:23). Kujikana nafsi humaanisha kumpatia Yesu utawala wa maisha yetu kila siku. Mtume Paulo anaelezea hivi, "Ninakufa kila siku" (1 Wakorintho 15:31).

Kama wanadamu tunapinga kujisalimisha, tukisahau kwamba "Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu" (2 Wakorintho 12:10). Tunapokea maisha ya kimwili wakati wa kuzaliwa, lakini bado tunakula kila siku ili kudumisha afya. Tunapokea maisha ya kiroho tunapozaliwa upya, lakini bado tunahitaji chakula cha kiroho kila siku la sivyo tutazidiwa na njaa ya kiroho na hatimaye tutakufa. Kama tusivyoweza kula milo yetu kwa ajili ya wakati ujao, vivyo hivyo hatuwezi kujisalimisha kwa Kristo kwa ajili ya kesho, tunahitaji kufanya hivyo kila siku. Ellen White anaandika kuwa, "Licha ya namna

tunavyojojiveka wakfu na kuwa kamili wakati wa badiliko, huko kujiwaka wakfu hakutatusaidia cho chote kusipofanywa upya kila siku" (*Our Father Cares*, uk. 144).

Jinsi ya Kuanza

Njia bora – na njia pekee – ya kupokea kila siku Roho Mtakatifu na kujisalimisha kwa yesu ni kuwa na ibada binafsi kila siku. Tusipomchagua Mungu kila siku, ahadi zetu na dhamiri zetu njema ni kama "kamba za udongo" (*Steps to Christ*, uk.47). Je, utajitoa leo katika kushiriki sehemu bora zaidi ya siku yako pamoja naye? "Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33).

Kuomba Neno la Mungu

Kudumu katika uhusiano bora zaidi uliopo

"Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu... Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa" (Yohana 15:4, 7).

Bwana, ahsante kwa kukuza imani zetu tunapojisalimisha kila siku kwako. Tuongoze kumfahamu Roho Mtakatifu vizuri ziadi. Hebu shauku zako zikawe ni shauku zetu.

Kuishi ndani ya uhusiano bora zaidi kila siku

"Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate" (Luka 9:23).

"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33).

Mpendwa Bwana, tufundishe kukutanguliza kwanza katika kila kitu. Tuonyeshe namna ya kuianza kila siku pamoja nawe.

Mapendekezo zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.

Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Mapendelekezo ya Nyimbo

Nina Haja Nawe (#126)

Uishi Ndani Yangu (#147)

Mtazame mwokozi (#212)

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamshowww.tendaysofprayer.org*Siku ya Saba***Kuomba Ahadi za Mungu**

Fungu Elekezi: “*Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa*” Mathayo 7:7.

Ushindi Usiowezekana Wawezekana

Yesu alitukomboa ili “tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani” (Wagalatia 3:14). Lakini ni kwa namna gani tunajenga imani yetu kwa kile alichoahidi? Ni kwa namna gani tunapaswa kuomba ili tuwe na uhakika wa kujazwa Roho Mtakatifu? Ni kwa namna gani moyo ulioamshwa huongoza katika ukuaji wa maisha halisi ya Kikristo?

Kwa miaka mingi nilifahamu maombi yaliyoitwa “kuomba na ahadi,” lakini kwa kipindi kirefu sijafanya kitendo hicho. Nilipotambua mibaraka ya kuomba ahadi za Mungu, nilitaka kushiriki na wengine. Miaka mingi iliyopita niliandika kitabu kilichoitwa *Hatua za Uamsho za Binafsi* (*Steps to Personal Revival*), kinachojumuisha sura inayohusu namna ya kuomba Maandiko kulivyo ufunguo kwa uzoefu wa maisha ya Kikristo kwa vitendo. Baadhi ya wasomaji walituma shuhuda hizi:

“Sikuwahi kufikiri ningeweza kupata ufahamu mpya kuhusu maombi – kuomba kulingana na ahadi za Mungu, kama ulivyoelezea. Wakati huu, Mungu amenipatia ushindi katika maisha yangu ambao sikuwahi kufikiri ungewezekana.”

“Tangu nilipojifunza kuomba na ahadi, maisha yangu yamebadilishwa... Mke wangu amegundua tofauti kamili ndani yangu. Pia, ninajishangaa.”

Jaribu Mwenyewe

Kuomba na ahadi humaanisha nini? Tunachagua ahadi ya Biblia au agizo Fulani katika Biblia, na kuomba maneno hayo kwa Mungu. Tunamtegemea kutenda kama alivyoahidi. Tunamruhusu atuongoze katika maombi yetu na kuzungumza nasi kupitia Neno lake. Na ikiwa tunahisi mashaka – kama inavyokuwa kwa kila mmoja nyakati fulani – tunaelekeza katika ahadi na kuzidai kama uhakikisho binafsi wa Mungu. Kadiri tunavyojaza mioyo yetu na maombi yetu kwa Maandiko, imani yetu inaimarishwa na hakika tunifahamu nia ya Mungu kuliko ilivyokuwa hapo kabla. Ellen White anaandika

kuwa, "Kufuta ahadi za Mungu kutoka katika Neno ingeweza kuwa kama kufuata juu kutoka katika anga... Mungu ameahdi katika Neno lake kwamba atatuongoza, na kwamba tumtumaini yeye. Kwa ahadi hizi anatuita tuondoe pazia kutoka katika umilele." (*My Life Today*, uk. 338)

Biblia inatupatia mwongozo ulio dhahiri kwa maombi yetu. Kwanza tunaambiwa tuombe kwa jina la Yesu: "Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya." (Yohana 14:14). Mungu pia ametupatia ahadi kwa wote kwamba anajibu maombi yanayoombwa kulingana na mapenzi yake: "Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba." (1 Yohana 5:14, 15). Mungu anadhihirisha nia yake katika maagizo yake pamoja na ahadi zilizopo kwenye Biblia, na tunaweza kumtumainia katika kufanya kile ambacho ameahidi. Aya ya 15 inasema kuwa, "Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba."

Maana ya maneno haya ni nini? Tunapoomba jambo Fulani tunalojua liko sawa na mapenzi yake, tayari ameshajibu wakati uo huo. Tunaweza kukosa kuona matokeo yanayoonekana mara moja. Na kwa kawaida hatutambui chochote kihisia. Lakini maombi yetu yanajibiwa kwa imani, siyo kwa hisia. Kwa kawaida hisia zinafuata baadaye, lakini kwa wakati uliopo, tunatumaini katika ahadi.

Kwa mfano, nimejifunza kitu Fulani ninapokuwa katika maombi na watu walio waraibu wa pombe na athari ya tumbaku. Wakati ule wanapoomba kwamba wafunguliwe kutoka katika vifungo vya uraibu, huwa hawawezi kutambua kitu. Ni lazima wafunguliwe kwa Imani. Lakini pengine baada ya saa kadhaa baadaye, wanagundua kwamba hawana ile hamu kali ya pombe au tumbaku. Wakati huo wanakuwa wamepokea majibu ya maombi yao kuhusu kufunguliwa. Maombi hayo yanakuwa yameshajibiwa kabla wao hawajatambua kwamba wamefunguliwa.

Ellen G. White pia anatoa utambuzi kuhusu kuomba kwa ahadi. "Mungu anafurahi watu wanapowasilisha madai kwake, ili wapate kutukuza jina lake. Wanaweza kutazamia mambo makubwa kama wana Imani katika ahadi zake." (*The Desire of Ages*, uk. 668). Jitahisi kusihi kwa dhati kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Mungu anasimama nyuma ya kila ahadi aliyotoa. Ukiwa na Biblia yako mikononi, anasema kuwa, Nimefanya jinsi ulivyosema. Ninawasilisha ahadi yako, "Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa;" (*Mathayo 7:7*) (*Christ's Object Lessons*, uk. 147).

Yesu anaahidi kuwa, "Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." (Marko 11:24). Je, unaomba ahadi zake kila siku? Tunapoomba kwa jina lake na kulingana na mapenzi yake, mbingu yote inasukumwa kufanya kitu!

Kuomba Neno la Mungu.

Mungu anasubiri kutupatia Roho Mtakatifu.

"Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" (Luka 11:13).

"Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa." (Yohana 7:39)

"Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtio." (Matendo 5:32)

Baba mpendwa, tunasoma kwamba utawapatia Roho Mtakatifu wale wanaokuomba, wale wanaokuamini, na wale wanaokutii. Hii ndiyo haja yetu. Tafadhali kamilisha hili katika maisha yetu, kwa sababu hatuwezi kufanya hivi sisi wenyewe. Ahsante sana kwa kumwagwa kwa upeno wako miyoni mwetu.

Anatukaribisha tujazwe na Roho

"Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho." (Waefeso 5:18)

Baba Mpandwa, tufundishe kudumu katika kukuomba na kwa kurudia kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu. Hatutaki tupungukiwe na Roho kama wale wanawali watano wapumbavu. Tujaze na hekima inayopatikana kwenye Neno lako.

Mapendekazo zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.

Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Sikiliza na kuitikia: Chukua muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa nyimbo na sifa.

Mapendeleko ya Nyimbo

Kumtegemea Mwokozi (#129)

Ahadi Tamu (#168)

Uliniimbie Tena (#139)

Nipe Biblia (52)

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamshowww.tendaysofprayer.org

Siku ya Nane

Utii Kupitia kwa Yesu

Fungu Elekezi: “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipyta; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.” 2 Wakorintho 5:17.

Hatua za Imani

Unakumbuka pale Yesu alipofanya muujiza wake wa kwanza kwenye harusi ya Kana ya Galilaya? “Mamaye akawaambia watumishi, Lo lote atakalowaambia, fanyeni.” (Yohana 2:5). Kwa kusema hivyo, Mariamu alijenga Imani ya watumishi kwa Yesu. Alipowaamba kujaza mabalasi kwa maji, walifanya jinsi alivyowaambia. Ndipo Yesu akawaambia kuwa, “Sasa tekeni, mkampelekee mkuu wa meza. Wakapeleka.” (Aya ya 8). Hapa pia walitii maagizo yake, hata kama ilionekana kama ni jambo lisilo la kawaida - na muda si mrefu wakagundua kwamba walikuwa wameshuhudia muujiza ukitendeka. Hebu rudi na kuangalia hatua moja moja tena:

1. Kwa maagizo yake Mariamu, alijenga **Imani ya watumishi kwa Yesu**
2. Watumishi walionesha Imani yao na utayari wao kwa kufanya kile ambacho Yesu aliwaagiza bila maswali. Kwa lugha nyingine, walichukua hatua ya **matayarisho** ambayo iliruhusu muujiza kufanyika.
3. **Ndipo Yesu akafanya muujiza peke yake.**

Watumishi hawakufanya lolote ili kugeuza maji kuwa divai - lakini unadhani muujiza ungetokea bila hatua zao za matayarisho? Hivi ndivyo utii wa Imani unavyotenda kazi: Tunachagua kumwamini Yesu, kuweka nia zetu kwake, kisha kuchukua hatua ya utii wa imani. Lakini Yesu - yaani Yeye peke yake - ndiye anayefanya miujiza.

Jinsi utendaji unavyotokea.

Mtume Paulo anaelezea kwamba siri imedhirishwa ndani yetu kwa kusudi maalum - ili kuleta utii na Imani. “Sasa na atukuzwe yeye awezaye kuwafanya imara, sawasawa na injili yangu na kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo, sawasawa na ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele, ikadhihirishwa wakati huu kwa maandiko ya manabii, ikajulikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu wa milele, ili waitii Imani. Ndiye Mungu mwenye hekima peke yake. Utukufu una yeye kwa Yesu Kristo, milele na milele. Amina.” (Warumi 16:25-27)

Hii ni siri gani? Kulingana na Wakolosai 1:27, ni "Kristo ndani yetu." Matokeo ya kupata utii kwa Imani katika Kristo ni nini? "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipyta; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya." (2 Wakorintho 5:17). Tunakuwa na maisha mapya Kristo anapoishi na kutenda kazi ndani yetu. Tunakuwa ni viumbe wapya!

Tunapokuwa na "Kristo ndani yetu" mwenendo wetu kuhusiana na amri zake unabadilika. "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito." (1 Yohana 5:3).

Yesu alisema kuwa, "kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi." (Mathayo 11:30).

"Nami nitajifurahisha sana kwa maagizo yako, Ambayo nimeyapenda. Sheria ya kinywa chako ni njema kwangu, Kuliko maelfu ya dhahabu na fedha. Mausia yako ni matamu sana kwangu, Kupita asali kinywani mwangu." (Zaburi 119:47, 72, 103).

"Wana amani nyingi waipendao sheria yako, Wala hawana la kuwakwaza." (Zaburi 119:165). Utii wa Imani, ni jambo la kupendeza kwa sababu Mungu katika upendo wake ametupatia sheria zilizo bora zaidi.

Pamoja na kwamba utii ni muhimu, utii huo hauwezi kununua wokovu, na utii hauwezi kutokea kwa sababu ya wema wetu. Ellen G. White anasema kuwa, "Yeye anayejaribu kuifikia mbingu kwa matendo yake mwenyewe katika kushika sheria anajaribu jambo lisilowezekana. Mwanadamu hawesi kuokolewa bila utii, lakini kazi zake hazitakiwi kuwa za kwake mwenyewe; inatakiwa Kristo afanye kazi ndani yake kunia na kutenda mapenzi yake yaliyo mema." (*Faith and Works* uk. 94). Dondoo tatu za kusisitiza:

1. Ni vigumu kuifikia mbingu kwa matendo yangu mwenyewe. Kujaribu kununua kitu kutoka kwa Mungu ni bure kabisa.
2. Hata hivyo, utii ni sehemu iliyo muhimu ya maisha na Mungu, kwa kuwa wafuasi wa Yesu wameitwa kuishi sawa sawa na mapenzi yake.
3. Utii hautakiwa kuwa ndiyo kazi yetu pekee, bali huu ni muujiza mkubwa uliokamilishwa ndani yetu na Kristo mwenyewe.

Tunashika nafasi gani?

Nirudie tena kwamba, hatuwezi kufanya jambo lolote ili tuweze kujiokoa wenyewe, bali Mungu anaheshimu ile hiari ya mwanadamu na anaruhusu tufanye chaguzi zetu

wenyewe. Kulingan na Ellen G. White, "Bwana amekusudia kwamba uwezo wa mbingu ushirikiane na jitihada za wanadamu." (*Mtapokea nguvu*, uk. 10). Hii maana yake ni nini?

1. **Tunatumaini.** Tunachagua kukuza matumaini yetu katika Kristo, ambaye anatenda ndani yetu kulingana na Wafilipi 2:13 "Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema."
2. **Tunaamua.** Ni lazima tuchague kutenda mapenzi ya Mungu. Na kwa sababu anaheshimu matakwa yetu na ile hali ya kufanya maamuzi binafsi, yeye ataingilia tu ikiwa tutafanya uamuzi. Anatusubiri tufanye hivyo.
3. **Tunachukua hatua ya matayarisho.** Tunaonesha maamuzi yetu kwa hatua ya utii, hatua ambayo inaweza kuwa kubwa au ndogo.
4. **Mungu pekee** ndiye anayefanya kazi kubwa ya wokovu ndani yetu.

Na kumbuka kwamba hata ile sehemu yetu tunayotenda – kumtumaini, kuamua, na kuchukua hatua ya matayarisho – inafanyika tu kwa uwezo wa Mungu, pale Yesu Kristo anapoishi ndani yetu kupitia kwa Roho Mtakatifu. Kufanya hivi kunatupatia utii na furaha.

Kuomba meno la Mungu

Utii unaturuhusu kupata uzoefu makamilifu wa upendo wa Mungu.

"Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake." (Yohana 14:21)

Baba, Ahsante sana kwa kutuonesha jinsi ya kupata maisha yaliyo bora kadiri iwezekanavyo. Tusamehe pale tunapokataa sheria zako na upendo wako. Tuongoze kukutumaini kikamilifu na kusalimisha moyo yetu yote kwako.

Mungu anafurahi pale tunapoomba atupatie moyo yenye utii.

"Kwa hiyo nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili niwahukumu watu wako, na kupambanua mema na mabaya; maana ni nani awezaye kuwahukumu hawa watu wako walio wengi? Neno hili likawa jema machoni pa Bwana, ya kuwa Sulemani ameomba neno hili. basi, tazama, nimefanya kama ulivyosema. Tazama, nimekupa moyo wa hekima na wa akili; hata kabla yako hapakuwa na mtu kama wewe, wala baada yako hatainuka mtu kama wewe." (1 Wafalme 3:9, 10, 12)

Bwana, tafadhali tupatie moyo yenye utii. Tupatie kutumaini kikamilifu katika uongozi wako, na kanuni zako hata pale tunapokuwa hatuelewi. Tufundishe kuona utii kupitia katika uwezo wa Roho Mtakatifu siyo kama mzigo bali kama jambo la kufurahia.

Mapendelezo zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.

Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Mapendelezo ya Nyimbo

Taamini Nitii Pia (#128)

Uniongoze Yehova (#157)

Nitembee Nawe (#14)

Bwana Uniongoze Juu (73)

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamsho

www.tendaysofprayer.org

Siku ya Tisa

Je, Ninafanya kazi kwa ajili ya Mungu – Au Yeye anatenda kazi kupitia kwangu?

Fungu Elekezi: “Nimesulibwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.” Wagalatia 2:20.

Kuumbwa kwa ajili ya Matendo Mema

Mwanafunzi wa Teolojia kutoka Austria aitwaye Zsolt alikatishwa tamaa. Alikuwa amekaribishwa kwenda kufanya uinjilisti katika nchi ya Kenya, lakini watu waliojitokeza walikuwa 30 tu lile juma la kwanza. Alikuwa ametumaini kuwa wangkuwa wengi. Akiwa amechanganyikiwa, alijifungia ndani ya chumba chake na kuomba kwa saa nne. Akimimina mashaka yake mbele za Mungu, alijisalimisha kikamilifu na akasubiri. Alikuwa na uhakika kwamba Mungu amesikia, ingawaje hofu na mashaka bado vilimsumbu. Ndipo jioni moja wakafika watu takribani 600. Siku iliyofuata wakaja 700, halafu wakaja 1,000. Mwisho wa mahubiri yale ya uinjilisti walibatizwa watu 39 kwa neema ya Mungu..

Kila tunapajaribu mambo makubwa kwa ajili ya mungu, tunakabiliana na swali muhimu sana kuwa, Je, ninafanya kazi kwa ajili ya Mungu kwa uwezo wa kibinadamu? Au Yeye ndiye anayefanya kazi kupitia kwangu kwa uwezo wake wa kimbingu?

Biblia inashughulikia hii siri ya jinsi Mungu anavyofanya kazi kwa uimara kupitia kwa ubinadamu ulio dhaifu. “Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.” (Waefeso 2:10). Aya hii inarejea katika kazi mbili: Kwanza Mungu “ametuumba katika Kristo Yesu.” Haya ndiyo maisha mapya aliyotupatia katika Kristo Yesu. Kasha Mungu anafanya kazi ya pili ndani yetu: “...tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.” Tutaishije ili kwamba Mungu afanye kazi hizi ndani yetu?

1. **Kuishi ndani ya Roho Mtakatifu:** “Hadi hapo watakapopokea Roho Mtakatifu, hawawezi kutambua kile ambacho Mungu anaweza kufanya kupitia kwao (*Ye Shall Receive Power*, uk. 286)

2. **Kuishi kwa kujisalimisha kikamilifu kwa Kristo:** "Yeye atakayejitoa kikamilifu kwa Mungu, huyo ataongozwa na mkono wa kimbingu... Kwa namna anavyothamini masomo ya hekima ya kimbingu, atakabidhiwa utume mtakatifu." (*The Acts of Apostles*, uk. 283, 284)

Kwa kukamilisa kazi ambayo Mungu ametuandalia, tunakua katika Imani, na uwezo wetu wa kiroho na kiakili unakuzwa Zaidi. Hata kushindwa kwetu kunakuwa na mafunzo ya thamani, kwa sababu tunajifunza kwamba hakuna jitihada za kibinadamu zinazoweza kuleta mafanikio bila kuwa na Mungu akiwa ndiye kitovu. Kuhubiriwa kwa Neno hakutakuwa na faida bila kuendelea kuwepo kwa msaada wa Roho Mtakatifu." (*The Desire of Ages*, uk. 671)

Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu

Na kwa namna wahubiri wanavyotakiwa kuwezeshwa na Roho wa Mungu, ndivyo ilivyo kwa waanzilishi wa mambo ya kiroho. "Ikiwa wokovu wa Mungu una yeye anayeandika andiko, roho huyo huyo ataonekana kwa mwandishi... Lakini kipande kilichoandikwa pale mwandishi anapokuwa haishi kikamilifu kwa utukufu wa Mungu, akiwa hakujitoa kikamilifu kwake, malaika wanahisi upungufu katika huzuni. Wanageukia mbali na hawaleti mguso wowote kwa msomaji kwa andiko hilo kwa sababu Mungu pamoja na Roho wake hawamo kwenye andiko hilo. Maneno ni mazuri, lakini yanakosa fukuto la mvuto wa Roho wa Mungu." (*EGW Letters and Manuscripts*, vol. 1 uk. 532).

Hii kanuni ni kweli kwa kazi zote, iwe ni huduma, mafundisho, au kuongoza mradi wa utume, ni uwezo wa mantiki ya kimbingu utendao kazi pamoja na mawakala wa kibinadamu ndiyo unaoweza kukamilisha kazi." (*Christian Service*, uk. 260)

Hata mwanadamu Yesu wa Nazareti alitegemea muunganiko wake na mbingu kila siku. Aliwauliza wanafunzi wake kuwa, "Hamsadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu? Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake." (Yohana 14:10). Au hebu tumwangalie mtume Paulo. Iliwezekanaje mtu mmoja kubeba kazi ya utume iliyokuwa kubwa kiasi hicho kisichoaminika? Alisema kuwa, "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." (Wagalatia 2:20). Paulo aliachia uhuru wake na kumruhusu Kristo aongoze maisha yake. Anaeleza kuwa, "Maana sitathubutu kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yangu, Mataifa wapate kutii, kwa neno au kwa tendo, kwa nguvu za

ishara na maajabu, katika nguvu za Roho Mtakatifu; hata ikawa tangu Yerusalem, na kando kando yake, mpaka Iliriko nimekwisha kuihubiri Injili ya Kristo kwa utimilifu;" (Warumi 15:18, 19). Ufunguo ni kuwa ndani ya Kristo.

Mungu anataka kufanya mambo makubwa hata leo hii. Mipango yake inavuka ng'ambo ya uwezo wetu. Ni kwa muunganiko wa maombi ya kudumu na yeye tu ndipo tunaweza kukamilisha jukumu letu kama alivyolitayarisha. Anaturalika kuwa "Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua." (Yeremia 33:3)

Kuomba Neno la Mungu

Uwezo wa binadamu unaweza kukamilisha matokeo ya kibinadamu.

"Musa akafundishwa hekima yote ya Wamisri, akawa hodari wa maneno na matendo. Alidhani kwamba ndugu zake watafahamu ya kuwa Mungu anawapa wokovu kwa mkono wake, lakini hawakufahamu. Huyo ndiye aliywatoa, akifanya ajabu na ishara katika nchi ya Misri, na katika bahari ya Shamu, na katika jangwa muda wa miaka arobaini." (Matendo 7:22, 25, 36)

Mpendwa Baba, tuongoze kujisalimisha kama Musa alivyofanya baada ya miaka yake ya uchungaji wa mifugo. Tunajua unaweza pia kutenda ishara na miujiza kupitia kwetu tunapokuwa tumeishi kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Hebu tufanye tuhiari kwenda pale unapotaka. Ahsante sana kwa uwezo wako wa kimbingu.

Tumeumbwa na Kristo kwa ajili ya matendo mema.

"Maana tu kazi yake, tuliumbwu katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo." (Waefeso 2:10)

Bwana, tufanye tuwe vyombo mikononi mwako kwa ajili ya wokovu na mibaraka kwa majirani zetu. Tunafahamu kuwa utimilifu wa injili unategemea katika swalii hili: Je, ninafanya kazi ya Mungu kwa uwezo wangu wa kibinadamu, au Mungu anafanya kazi kupitia kwangu kwa uwezo wake wa kimbingu? Hebu tufundishe kwamba hatuwezi kukutumikia kwa uwezo wetu wenyewe. Ahsante kwa kutuahidi kwamba utafanya kazi kupitia kwetu. Tafadhali bariki kazi ya mikono yetu.

Mapendelezo zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.

Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Mapendelezo ya Nyimbo

Twae Wangu Uzima (#146)

Po Pote Na Yesu (#133)

Alilipa Bei (#119)

Nasikia Sauti yako (142)

Siku kumi za Maombi 2021 – Kutafuta Uamshowww.tendaysofprayer.org*Siku ya Tisa***Kutafuta Uamsho Pamoja**

Fungu Elekezi: “Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi.” (Zakaria 4:6).

Ni nini kinachofuata? Hatua tatu za kuanza kiroho

Je ungependa kupitia uzoefu wa uamsho wa kiroho pamoja na familia ya kanisa lako? Hapa pana mpango mmoja unaopendekezwa ambao umeongoza katika uamsho wa kiroho na tumaini kwa makanisa kule Ujerumani, Uswisi, Uingereza, Tajikistan, na Marekani. Uamsho unawenza kufanyika popote, hata katika nchi zisokuwa za kidini, watu wanapoendelea kujisalimisha kwa Yesu na kumwomba mibaraka ya Roho Mtakatifu.

omba kuhusu jinsi kanisa lako, familia yako au kikundi chako cha maombi kinavoweza kupata uzoefu wa “Kuanza upya” kiroho mwaka huu. Andaa mpango, tafuta mchango wa mawazo kutoka kwa wengine, na amua tarehe ya kuanza. Utataka kukubali mawazo kutegemea na utamaduni wako, jumuia yako, na mahitaji ya kikundi chako.

Tunataka kushiriki mfano wa kanisa moja la Decatur, kule Alabama Marekani.

1. Anza Upya

Tenga majuma kadhaa au miezi ya kuomba Roho Mtakatifu kwa kina, wakati huo huo ukisoma Maandiko na ikiwezekana kitabu kidogo cha kesha.

Katika matayarisho ya mfululizo wa mahubiri ya uinjilisti, washiriki wa kanisa la Decatur walianza kwa kuomba pamoja kanisani kwa dakika kama 30 kila Sabato asubuhi. Walishiriki vielekezi vilivokuwa kwenye kijarida cha matangazo ya kanisa ili kuhimiza maombi, uamsho, na kazi ya Roho Mtakatifu. Waliendesha pia semina ya video kuhusu Roho Mtakatifu Sabato mbili nyakati za jioni. Baada ya semina, walisambaza vitabu vidogo kuhusu umsho wa kiroho na wakawaelekeza washiriki kuvisoma kwa kipindi cha majuma sita yaliyofuata. (Walichagua kijitabu cha ‘*Hatua Kuelekea katika Uamsho.*’ Mapendekezo mengine yalikuwa kijitabu cha ‘*Jipatie Amani*

Moyoni.' Au mwongozo wa kujifunza Biblia kuhusu uamsho.) Baadaye, katika kipindi cha siku kumi za maombi, waliomba kwa ajili ya uamsho na Roho Mtakatifu, na wakasherehekea Sabato ya Maombi na Sifa.

2. Kujali mahusiano

Kuanza maombi ya upatanisho kwa ajili ya watu watano ambao bado hawajafikiwa, kisha wasiliana nao na kudumisha urafiki kwa namna ambayo haina unafiki na kwa uangalifu sana. Katika kipindi chote hiki unaweza kutaka kujifunza kitabu kingine kuhusu maombi au uamsho. Kusudia kujifunza katika hali ya wawili wawili ili kutegemeza uelewa kwa kina.

Katika kipindi hiki cha awamu ya pili, washiriki wa kanisa la Decatur walianza kujifunza kitabu cha *40 Days: Prayer and Devotion to Prepare for the Second Coming* (Siku 40: Maombi na Ibada katika kujitayarisha kwa ajili ya kurudi mara ya pili) wakiwa katika vikundi vyta wawili wawili. Matokeo yake ni kwamba furaha yao katika kuwaambia wengine kumhusu Yesu iliongezeka. Kama vile ilivyopendekezwa katika kitabu, washiriki pia walianza kuomba kwa ajili ya watu watano ambao hawajawafikia bado katika maisha yao. Baada ya hapo waliwasiliana na wale waliokuwa wamezoeana nao katika makanisa yao ya awali na kuendeleza mawasiliano kwa muda kidogo. Matokeo yake yalikuwa ni ubatizo na mibaraka kwa washiriki wote, wale wa wapya, pamoja na wale waliokuwa wakiwaombea.

Hebu fikiria kuhusu hili. Ikiwa washiriki 10 wa kanisa kila mmoja atawaombea watu 5 na kudumisha mawasiliano nao. Hao watakuwa watu 50, na idadi itaanza kuongezeka kuanzia hapo. Mwisho wa siku 40, unaweza kukaribisha watu wale uliokuwa ukiwaombea katika Sabato maalum ya wageni. Baada ya hapo utakuwa unakaribisha kila mmoja wao kujiunga katika kikundi kidogo cha kujifunza Biblia (Mkijifunza Bibilia, mapishi yenye afya, mazoezi, shughuli za kijamii, au chochote kitakachoonekana kufaa kwa watu wenye shauku inayofanana). Unaweza pia kuwakaribisha katika mikutano wa uinjilisti unaofuata. Kumbuka kuhudhuria mikutano na rafiki zako na kuwasaidia kujisikia wanakaribishwa.

3. Kushiriki

Kila mshiriki anaweza kukaribisha watu ambao amekuwa akiwaombea ili wahudhurie mikutano ya kiinjilisti, au katika vikundi vidogo vyta kujifunza Biblia, au hata masomo ya kujifunza mtu mmoja na mwenziwe. (Ikiwa baadhi ya wale unaowaombea wako tayari kwa ajili ya mafundisho ya Biblia, wakaribishe

katika kikundi kidogo kinachojielekeza katika eneo fulani la mvuto, kama vile mazoezi, mapishi ya afya, jambo alipendalo mtu analofanya wakati wa kupotezea muda au shughuli ya kijamii.)

Kanisa la Decatur lilipoendesha mfululizo wa mahubiri ya uinjilisti, washiriki wake walipata uzoefu wa uamsho na uhusiano wa kina na Yesu. Roho Mtakatifu alifanya kazi miyoni mwa wageni waliokuwa wamealikwa, na watu 10 walitoa maisha yao kwa Yesu na kubatizwa (na wengine watano zaidi wakijiunga hapo baadaye). Matokeo yalikuwa ni ushuhuda wa uwezo wa maombi! (Kisa cha Decatur kimetolewa katika taarifa na Elida Meneses wa *Southern Tidings*.)

Je, kanisa lako linaweza kufanya nini?

Ombeni pamoja na kupanga kwa ajili ya kanisa lenu leo. "Mbingu yote iko katika shughuli, na malaika wa Mungu wanabiri kushirikiana na wale wote watakaoandaa mipango kwa namna ambayo zile roho ambazo Yesu alizifia zitapata kusikia habari njema ya wokovu. Malaika ambao wanawahudumia wale ambao watakuwa warithi wa wokovu, wanawaambia watakatifu wote kwamba kuna kazi kwa ajili yenu ya kufanya, 'Enendeni mkasimame hekaluni mkawaambie watu maneno yote ya Uzima huu.'" (Matendo 5:20) (*Testimonies for the Church*, vol. 6, uk. 433, 434)

Mungu anakutuma uende ulimwenguni ukiwa na ahadi hii: "Kile unachopanga hakitafanikiwa kwa uwezo wa majeshi yenyе nguvu za kibinadamu, bali kwa Roho yangu ndipo watafanikisha kile wanachopanga. "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi." (Zakaria 4:6)

Kuomba kwa Neno la Mungu.

Roho Mtakatifu atalikamilisha.

"Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi."

Mpendwa Baba, Unatuambia kwamba mafanikio hayaji kuitia katika jitihada za mwanadamu. Tafadhali tusamehe kwa kukosa kwetu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Leta uamsho kwetu ili tusiendelee kuwa uvuguvugu kama Laudikia. Tuamshe kwa ajili ya wokovu wetu wenywewe na wa wale majirani zetu. Na ahsane sana kwa ajili ya furaha ya milele ambayo umetuaahidi.

Mapendelezo zaidi ya Maombi

Shukurani na Sifa: Shukuru kwa mibaraka mahususi na msifu Mungu kwa wema wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na msifu Mungu kwa msamaha wake.

Uongozi: Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Muombe Mungu abariki jitihada za kanisa letu mahalia, ngazi ya kanisa ya kanda, na ngazi ya kanisa kiulimwengu.

Mahitaji ya eneo mahalia: Ombea mahitaji ya washiriki wa kanisa, familia, na majirani.

Sikiliza na Itika: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa au wimbo.

Mapendelezo ya Nyimbo

Twapanda Mapema (#55)

Mpaka Lini Bwana (#78)

Hadithia Kisa cha Yesu (#34)

Baba Anilinda (131)



KANISA LA
WAADVENTISTA WA SABATO

“Nanyi mtanitafuta na
kuniona, mtakaponitafuta
kwa moyo wenu wote.”

Yeremia 29:13

Mtafsiri: Moseti Chacha
P.O. Box 2443 Arusha, Tanzania
Simu: +255 712 282 224 / 756 449 399
moseti.chacha@gmail.com